# Nipashe

Jumatatu Mei 25, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580240

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

MWANGA WA JAMII




## Ndege za watalii zatua, rubani, watalii walonga

UK. 3




UKURASA 11

# Walichoteta JPM, Maalim Seif Ikulu

**MAZUNGUMZO** yagusia kutangazwa mshindi halali Uchaguzi Mkuu Zanzibar... *Endelea UK. 2*



Baadhi ya waumini wa dini ya Kiislamu wakishiriki swala ya Eid El Fitri, katika msikiti wa Nughe, jijini Dodoma jana. Picha zaidi uk.18. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH** .

## Serikali yataja siri corona kupungua

■ Dk. Shein aeleza ilivyobadili mfungo... *Uk. 2, 17*

## BAA LA CORONA



Nchi nyingi duniani zimeathirika na ugonjwa wa corona ambao umesababisha vifo, na familia kubaki yatima. Huwezi jua lini na wapi utaupata ugonjwa huo. Tahadhari zinapaswa kuchukuliwa katika kipindi chote ili kujikinga na janga hili. WHO

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## WABUNGE WAIJIA JUU BANDARI MAPATO

UKURASA 5





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** SIMBA SC YAANIKA MKAKATI WA USAJILI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Walichoteta JPM, Maalim Seif Ikulu

**Na Enock Charles**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeanika walichoteta Rais John Magufuli na Mwenyekiti wa chama hicho, Maalim Seif Sharrif Hamad.

Machi 3 mwaka huu, Maalim Seif alizuru Ikulu jijini Dar es Salaam na kufanya mazungumzo na Rais Magufuli. Hata hivyo, haikuelezwa walichoteta wawili hao.

Nipashe iliyopata nafasi ya kuzungumza kwa faragha na Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, mbali na mambo mengine ilitaka kufahamu walichozungumza Maalim Seif na Rais Magufuli Ikulu.

Gazeti hili pia lilitaka kufahamu kama ziara hiyo ya Maalim Seif Ikulu ilikuwa na ridhaa ya ACT-Wazalendo na kama aliwasilisha mrejesho kwa chama kuhusu kile alichoteta na mkuu wa nchi.

Shaibu alisema kuwa katika mazungumzo yao, wawili hao walijadiliana mambo mengi, ikiwa ni pamoja na mchakato wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo alisema Rais Magufuli alikihakikishia chama hicho kuwa mshindi halali atatangazwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, ikiwamo nafasi ya urais Zanzibar ambayo uchaguzi mkuu uliopita iliibua mvutano mkubwa wa kisiasa nchini.

Kwa kutambua hali ya siasa ya Zanzibar, Shaibu alisema kuwa Maalim Seif alipokwenda Ikulu, walizungumza kwa kina na Rais Magufuli kuhusu mwelekeo wa siasa za visiwa hivyo.

"Mwenyekiti wetu (Maalim Seif) alitueleza kuhusu kile alichozungumza na Rais Magufuli na kwa kiasi kikubwa (mazungumzo yao) yalijikita katika hali ya kisiasa Zanzibar.

"Rais amemhakikishia kwamba uchaguzi wa Zanzibar utakuwa huru na wa haki na kwamba Rais Magufuli atahakikisha kwamba anayeshinda, anapewa serikali. Haya ni mambo ambayo sisi kama chama yanatupa faraja," alisema.

Shaibu alisema kutokana na umuhimu wa Maalim Seif katika siasa za Zanzibar na umoja wa kitaifa katika visiwa hivyo, ni muhimu kuilinda amani na utulivu ulioko katika visiwa hivyo kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

"Maalim amebakia kuwa 'key player' katika siasa za Zanzibar tangu kuanzishwa kwa vyama vingi, kwa sababu licha ya matokeo kuonyesha kuwa kuna mbinu za kumpoka ushindi, hajachukua hatua, ukiacha mwaka 2001, kuwaingiza watu barabarani," Shaibu alisifu.

Mwaka 2015, Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ililazimika kubatilisha matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huo kwa upande wa urais wa Zanzibar na kuurudia.

Tume hiyo iliyokuwa chini ya uenyekiti wa Jecha Salim Jecha, ilichukua uamuzi huo baada ya Maalim Seif, aliyekuwa mgombea wa urais kupitia Chama cha Wananchi (CUF), kujitangaza mshindi kabla ya kutangazwa na tume.

Vyama vyote vilivyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) vilitangaza kususa kushiriki uchaguzi wa marudio, ambao licha ya kususa kwao, ulifanyika na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutangazwa mshindi.

CUF, moja ya vyama vilivyokuwa Ukawa, ilitangaza kutoutambua uchaguzi huo kusisitiza mshindi atangazwe kupitia uchaguzi uliofanyika awali badala ya kufanyika kwa uchaguzi mwingine na baadaye kutoutambua ushindi wa Rais wa sasa wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein.

CUF na Ukawa waliendelea na msimamo wao huo wa kutoutambua urais wa Dk. Shein, wakisusa kushiriki shughuli kadhaa zilizomhusisha, ukiwamo ufunguzi wa Bunge la 11 mjini Dodoma, ambao wabunge wa vyama hivyo walitoka ukumbini baada ya Rais Shein kuingia.

Maalim Seif (76), amekuwa mpinzani mkuu Zanzibar tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini mwaka 1992 na amekuwa akishika nafasi ya pili katika matokeo ya urais visiwani humo kila unapofanyika uchaguzi.

Amewahi kushika nafasi mbalimbali katika visiwa hivyo ikiwamo ya Makamu wa Kwanza wa Rais.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwahutubia waumini wa dini ya Kiislamu, baada ya swala ya Eid el Fitri, katika Msikiti wa Gaddafi, jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM** .

## Serikali yataja siri corona kupungua

**Peter Mkwavila na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema kupungua kwa maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha homa kali ya mapafu, kumetokana na Watanzania kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya.

Majaliwa aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waumini wa dini ya kiislamu katika ibada ya sikukuu ya Eid el Fitr iliyofanyika Msikiti wa Gadaffi jijini hapa.

Alisema wagonjwa wa corona nchini wamepungua kwa kiasi kikubwa tofauti na ilivyokuwa awali kutokana na Watanzania kutekeleza maagizo ya wataalamu wa afya na kumwomba Mungu.

Majaliwa alisema ugonjwa huo ambao kwa sasa ni tishio duniani, umeitikisa Tanzania na mataifa mengine, lakini kutokana na maombi ya viongozi wa dini na waumini na msimamo wa serikali iliyokuwa ikitolewa, umepungua kwa kiasi kikubwa zaidi.

"Sisi kama serikali tunawashukuru Watanzania kwa ujumla kwa kuomba mbele za Mungu pamoja na tahadhari ambazo zinachukuliwa ikiwa kwa kunawa maji chirizika na sabuni na kupakaa vitakasa mikono na kuvaa barakoa na ndiyo maana hatuna budi kusimama na kusema ugonjwa huu kwa kweli umepungua kwa kiasi kikubwa," alisema.

Waziri Mkuu aliwataka Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo kwa kuendelea kuvaa barakoa, kunawa kwa maji tiririka na kujiepusha na misongamano.

Kiongozi huyo wa serikali pia aliwaomba viongozi wa dini kuendelea kumwomba Mungu na kuhamasisha amani, ili nchi isije kuingia katika machafuko ya aina yoyote.

"Tanzania ni nchi ya mfano katika Bara la Afrika na duniani kwa ujumla kutokana na kuwa na amani, upendo na ushirikiano na hiyo inatokana na ukweli kuwa watangulizi wa taifa waliweza kujenga umoja, ushirikiano na upendo, hivyo kuna umuhimu mkubwa sana wa kuendelea kujenga misingi hiyo kwa vizazi na vizazi," alisema.

Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Alhaji Mustapha Shabani, aliwataka waumini wa dini ya kiislamu kuitumia vyema sikukuu hiyo kwa kuyatafakari matendo makuu ya Mungu na wasijiingize katika anasa ambazo zinaweza kupoteza dhana nzima ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

"Ninawaomba waumini wenzangu tusiwe kama wafungwa ambao baada ya kufunguliwa kwenye kifungo, wakaona ndiyo nafasi yao ya kufanya maovu tena kutokana na walivyokuwa ndani ya jela kuonekana kuzikosa anasa hizo," alisema.

Aliwasisitiza kuendelea na maombi ili ugonjwa wa corona utokomee kabisa.

"Tunatakiwa kuendelea kumshukuru Mungu na kumwomba ili kuondosha kabisa ugonjwa huu, huku hali ya kuchukua tahadhari zinazotolewa na wataalamu wa afya ikizingatiwa pamoja na kuondokana na mikusanyiko isiyokuwa ya lazima," alisema.

Katika hatua nyingine, wito umetolewa kwa Waislamu kuwa na matendo mema kama walivyofanya wakati wa mfungo wao.

Akitoa mawaidha katika ibada ya sikukuu hiyo, Sheikh wa Msikiti wa Nughe, Omari Salimu Itara, aliwataka kuendelea kutenda mema huku wakizingatia maelekezo ya kujikinga na maambukizo ya corona.

"Rais John Magufuli aliagiza kufanyika kwa maombi maalumu siku ya leo (jana) ya kumshukuru Mungu kwa kuendelea kutulinda na kutuepusha na ugonjwa wa corona, hivyo tusisahau kuendelea na maombi hayo hata tukiwa majumbani kwetu," alisema.

Sheikh huyo alisema wakati wa mfungo watu walijizuia kutenda mabaya, hivyo waendelee kutenda mema kila siku katika jamii yao.

"Ninajua wakati wa mwezi huu, watu walijizuia kufanya mabaya, lakini sasa ninajua tumefungua, wengine wanaona kama Mungu hawaoni, la hasha anatuona kila wakati, hivyo hakikisheni mnakuwa katika utulivu huo," alisema.

Aliwataka waaumini hao kusherehekea sikukuu kwa kutulia nyumbani na familia zao, ili kujiepusha na maambukizo ya ugonjwa huo.

Kwa upande wake, Imamu wa msikiti huo, Sheikh Abdul Musa Kondo, aliwataka waaumini hao kuendelea kuzingatia kutumia barakoa na vitakasa mikono wakati wa kuingia na kutoka, ili kujikinga.

Sheikh Kondo alisema waumini hao pia wanatakiwa kuendelea kusali kwa kuachiana nafasi kama ilivyoshauriwa na wataalamu wa afya.

Machi 16 mwaka huu, Tanzania iliripoti mgonjwa wa kwanza wa corona na siku moja baadaye ilitangaza kufunga shule na vyuo vyote nchini ikiwa ni hatua mojawapo ya kudhibiti kuenea kwa virusi hivyo hatari.

Mpaka sasa, nchi imeripoti kuwa na visa 509 na vifo 21 vya corona, huku watu 183 wakipona.

Hadi jana saa 10:19 jioni, kulikuwa na visa 5,434,617 na vifo 344,504 vya corona, huku 2,273,150 wakipona duniani.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya (kushoto), akitoa ufafanuzi kuhusu juhudi zilizofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) kuhusu uzalishaji wa zao la miche ya michikichi katika shamba la Gereza la Kwitanga, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, juzi. Kulia ni viongozi wa Tari na taasisi nyingine za kilimo. **PICHA: ASHTON BALAIGWA.**

# Mtoto auawa kwa sumu, mdogo wake anusurika

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MTOTO mdogo anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka minane amefariki dunia, huku mwenzake akiendelea kupata matibabu katika Kituo cha Afya Sirari wilayani Tarime Mkoa wa Mara, baada ya kulishwa chakula kinachosadikiwa kuwa na sumu.

Tukio hilo lilitokea Jumamosi katika Kijiji cha Ng'ereng'ere ambapo inadaiwa mtu asiyefahamika alifika nyumbani kwao majira ya asubuhi wakati wazazi wao walikuwa wametoka kuelekea katika shughuli za biashara katika soko kuu la mjini Sirari.

Watu walioshuhudia tukio hilo walisema wasamaria wema na majirani walifika katika eneo la tukio mita chache kutoka katika stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani baada ya kusikika makelele ya kuomba msaada.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ng'ereng'ere, Chacha Ghati, alisema wananchi waliwafikisha watoto hao katika kituo hicho cha afya, huku alionekana kuzidiwa na kuamriwa apelekwe katika chumba cha wagonjwa mahututi, lakini alifariki dunia muda mfupi baadaye.

Alisema kwa mujibu wa taarifa ya uchunguzi wa chanzo cha kifo iliyotolewa na madaktari wa kituo hicho, alifariki kutokana na kubugia kiasi kikubwa cha sumu, na wataalamu bado wanachunguza aina ya sumu hiyo.

Alisema ataitisha mkutano wa dharura wa kijiji kwa ajili ya kuendesha zoezi la kupigwa kura za siri kwa kushirikisha Jeshi la Polisi ili kubaini watu au kikundi chochote kilichohusika na kupanga mauaji hao.

Mzazi wa watoto hao, Nyankogoti Masaite, alisema mtoto wake aliyepoteza maisha alikuwa anasoma darasa la pili katika shule ya Ng'ereng'ere, huku mwingine mdogo aliyenusurika anasoma chekechea, na kwamba aliruhusiwa kutoka hospitali jana.

# Ndege za watalii zatua, rubani, watalii walonga

**Asraji Mvungi, ARUSHA**

NDEGE kutoka mataifa mbalimbali, zimeanza kuwasili nchini zikiwamo za watalii ikiwa ni siku sita baada ya serikali kutangaza rasmi kuondoa zuio la ndege kutua nchini kutokana na baa la corona.

Ndege zilizowasili zikiwa na watalii ni pamoja na zinazotoka Marekani na Afrika Kusini, zilizoingia nchini kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Nipashe ilishuhudia mwishoni mwa wiki moja ya ndege kutoka Marekani ikitua KIA ikiwa na watalii wanne ambao baada ya kukamilisha taratibu za kiafya, walianza safari ya kwenda kuangalia vivutio katika maeneo mbalimbali, ikiwamo Hifadhi ya Ngorongoro.

Nipashe pia ilishuhudia kundi lingine la watalii kutoka Afrika Kusini ambao pia wamekuja kwa ajili ya kutembelea vivutio vya Tanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuwasili KIA, mmoja wa watalii kutoka Afrika Kusini, Tracu Stanley, alisema amefurahi kupata fursa kutua Tanzania kujionea vivutio naameridhishwa na tahadhari za kiafya zinazochukuliwa katika kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona.

"Tunafurahi na kushukuru kwa kupata fursa hii ya kuja Tanzania nchi nzuri na yenye vivutio vingi," Stanley alipongeza.

Rubani wa ndege iliyokuja na watalii kutoka Marekani, Rob de Man, pia alieleza furaha yake kutua Tanzania kipindi hiki ambacho dunia ina hofu ya corona, akipongeza pia tahadhari zinazochukuliwa na nchi kukabiliana na janga hilo.

Siku chache baada ya kuripotiwa kwa mgonjwa wa kwanza corona nchini, serikali ilitangaza kulifunga anga lake kwa kukataza ndege kutua nchini, ili kukabiliana na baa hilo.

Hata hivyo, baadaye Mei 18 mwaka huu, serikali ilitangaza kufungua anga lake na kuruhusiwa ndege za aina zote kuanza kutua nchini.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, akiongea na waandishi wa habari wiki iliyopita mjini Dodoma, alisema kuwa pamoja na anga kufunguliwa, hadhari dhidi ya homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19) inaendelea kuchukuliwa.




**Bonite Bottlers Ltd** inayo furaha kuwaletea **Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa wa LITA 6, LITA 12 na LITA 18.9.** Tumewekeza katika mitambo ya kisasa ya kuzalisha maji katika ujazo mkubwa ili kuwawezesha wateja, wanywaji na wadau wetu kupata maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, maofisini na kwenye taasisi mbalimbali.

**UPATIKANAJI:-**

- Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa yanapatikana kwenye depoti zetu zote zilizoko mikoani, maduka na wauzaji wa jumla nchi nzima.
- Kwa Wateja wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam, unaweza kununua maji ya kunywa ya Kilimanjaro ukiwa nyumbani kwa njia ya mtandao kupitia makampuni ya usambazaji bidhaa tunayoshirikiana nayo ambayo ni **Shoponline Tanzania www.shoponline.co.tz** na Piki Deliveries **www.piki.co.tz** .

Ni matumaini yetu mtaendelea kutuunga mkono kwa kuburudika na maji kutoka kilele cha Afrika.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI:**

**Moshi:** +255 755851170 au +255 27 2754422/7, **Arusha:** +255 756339532 au +255 27 2544876, **Dar:** +255 754635988 au +255 22 700450/655, **Morogoro:** +255 782546090, **Dodoma:** +255 787495439, **Karatu:** +255 757673123, **Babati:** +255 765459199, **Singida:** +255 755271963, **Tanga:** +255 763407979, **Mbeya:** +255 757266235, **Mwanza:** +255 742099191, **Nzega:** +255 746031412

**MAJI YA KUNYWA YA KILIMANJARO NI MAJI YA KUAMINIKA KILA SIKU!**

# Imamu amfagilia Rais vita corona

**Na Francis Godwin,** IRINGA

IMAMU msaidizi wa msikiti wa Furqan Kihesa mjini Iringa, Abdulaziz Isihaka, amesema maamuzi ya Rais John Magufuli katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona yameshangaza dunia.

Amesema kupitia maamuzi yake ya kutozuia wananchi kutoka nje, dunia nzima inamuona ni mwenye maono.

Akizungumza baada ya ibada ya Idd, Imamu Isihaka alisema kitendo cha Rais Magufuli kutozuia wananchi wake kutoka nje wakati wote wa janga la maambukizo ya corona si tu kimepongezwa na Watanzania bali kimelipatia heshima kubwa Taifa kuwa na kiongozi mwenye maono ya Kimungu katika kuongoza wananchi wake, kwani kiongozi mwenye maono ya Kimungu hatumii nguvu katika kuongoza wananchi wake.

Alisema wakati nchi nyingine za Afrika na duniani zikitumia nguvu kubwa kuzuia wananchi wake kutoka nje, kwa Tanzania ilikuwa tofauti kwa serikali kuwaruhusu wananchi wake kuendelea na majukumu yao ya kila siku, huku wakichukua tahadhari kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya.

"Jambo ambalo leo kila mmoja wetu anashuhudia nchi... zilizofungia wananchi wake ndani ndivyo zenye vifo vingi, tena si vifo vya corona bali ni vinavyotokana na vurugu za kulazimisha watu kutotoka nje," alisema kiongozi huyo.

Imamu alisema kuwa uislamu unaelekeza kuwa yanapotokea magonjwa ya maambukizo, mara nyingi kuna kuwa na karantini na wakati wa Mtume kulikuwa na ugonjwa hatari sana wa tauni uliosababishwa na panya, ambapo Mtume aliwaambia wale waliopo nje ya mji wenye maambukizo wasiingie ndani ya mji usio na maambukizo na waliopo ndani wasitoke nje ili kuzuia maambukizo zaidi.

"Kuwa hiyo ililenga kuthibiti maambukizo zaidi, kwani karantini haijaanza leo wakati wa janga hili la corona ilikwisha kuwapo miaka hiyo ila kwa Tanzania tunamshukuru sana Rais Magufuli kwa kuishi katika hali ya kumtanguliza Mungu zaidi kuliko kitu chochote kingine."

Imamu Isihaka alisema kuwa uamuzi wa Rais Magufuli wa kuruhusu shughuli mbalimbali ziendelee na vyuo kufunguliwa ni sahihi sana kwani kufunga shughuli hizo pasipo kujua mipango ya Mungu ni kutesa bure wananchi.

# Kabudi atetea kauli ya JPM corona kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imeitaka dunia na Jumuiya za Kimataifa kutambua kuwa kauli ya Rais John Magufuli kuwahimiza Watanzania kusali na kuliombea Taifa kuondokana na maradhi ya Covid -19 haikuwa kauli ya kupuuza kanuni za kisayansi za mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Akitoa salamu za shukrani kwa Mungu na Watanzania kwa niaba ya Rais Magufuli ikiwa ni hitimisho la siku tatu za kumshukuru Mungu baada ya maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa homa kali ya mapafu Covid -19 kupungua nchini katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Albano Dayososi ya Dar es Salaam jana, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema licha ya kauli ya Rais kutaka Watanzania kusali bado serikali ilisisitiza kufuatwa kwa kanuni za kisayansi za kuepuka maambukizo ikiwa ni pamoja na kuvaa barakoa, kunawa mikono na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

Aliongeza kuwa hatua ya Tanzania kufunga maabara yake iliyokuwa ikipima virusi vya corona hapo awali kabla ya Rais Magufuli kubaini kasoro katika maabara kuu, hatua hiyo iliifanya Tanzania kuchukua hatua ya kujijengea uwezo wake wa ndani na kujenga maabara mpya yenye uwezo wa kuwapima watu wanaodhaniwa kuwa na virusi vya corona maradufu.

Prof. Kabudi alisema kupitia kwa waumini wa kanisa hilo, alisema Rais Magufuli anashukurani kubwa sana kwa Mwenyezi Mungu na kwa Watanzania wote kwa kuitikia wito wake wa wananchi kuondokana na hofu na badala yake wamlilie Mungu, jambo ambalo maombi hayo yamejibiwa kwa kupungua maambukizo licha ya uwapo wa ubashiri juu ya idadi ya watakaoathirika na kufariki dunia kwa maradhi ya Covid-19 kufikia 100,000 kwa Tanzania pekee.

Akizungumza wakati wa mahubiri Canon Francis Xavery kwa upande wake, alimshukuru Rais Magufuli kwa uamuzi wake wa kutofunga nyumba za ibada, yakiwamo makanisa na misikiti licha ya mashinikizo kutoka sehemu mbalimbali, jambo lilimfanya Mwenyezi Mungu kusikia maombi ya Watanzania kwa kuwa walimwamini Mungu.

Padri Jacob Kahemele wa Kanisa la Kuu la Mtakatifu Albano Dayosisi ya Dar es Salaam, alisema kanisa hilo limeungana na waamini nchini kote kuitikia rai ya Rais, huku akiwataka Watanzania kuacha kujipa hofu hususani katika mambo ambayo yanapita upeo wa binadamu na badala yake kila mmoja kwa imani yake kujinyenyekeza mbele ya Mungu ambaye ni suluhisho la mambo yote yanayoonekana na yasiyoonekana.



Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza nchini, Suleimani Mzee, akikata utepe katika uzinduzi wa nyumba mbili za watumishi Shule ya Sekondari Bwawani, inayomilikiwa na jeshi hilo, mkoani Morogoro juzi. **PICHA: FRANK KAUNDULA.**

# Bosi Magereza abainisha malengo kwa watumishi

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

KAMISHNA Jenerali wa Jeshi la Magereza nchini, Suleimani Mzee, amezindua nyumba mbili za watumishi na gari moja la Shule ya Sekondari Bwawani inayomilikuwa na jeshi hilo, mkoani Pwani, ambavyo vyote vimegharimu zaidi ya Sh. milioni 190.

Akizungumza baada ya makabidhiano hayo juzi, Kamishna Jenerali Mzee aliwataka watumishi wa jeshi hilo kuhakikisha wanabadili mitazamo yao na kuelekeza nguvu katika ubunifu wa miradi mbalimbali itakayowawezesha kujiendesha wenyewe.

Alisema Jeshi la Magereza kwa sasa linalenga kufika hatua ya kuwa taasisi inayoweza kujitegemea yenyewe, ambapo njia sahihi ni watumishi wake kubuni miradi mbalimbali, huku akiwataka watumishi wa jeshi hilo, kuamini katika kufikia azma hiyo.

"Kila mmoja wetu akiamini kwamba tunaweza kwa kubuni miradi tutafika mbali kwa sababu hatuwezi kuendelea kuwa tegemezi wakati tuna rasilimali zote muhimu na miundombinu wezeshi ipo... tunakosa kujiamini tu kwa baadhi ya watumishi," alisema Mzee.

Hata hivyo, aliupongeza uongozi wa shule hiyo kwa jitihada zilizofanywa kwa ubunifu wa miradi na kuwataka kuweka mikakati ya kufungua matawi katika shule hiyo katika mikoa mingine.

Kwa upande wake Mkuu wa Shule hiyo, Anthony Sogoseye, alisema wanaendeleza mikakati ya kuboresha taaluma inayotolewa kwa kuboresha, miundombinu ya usomaji, nyumba za watumishi ili kuongeza wanafunzi zaidi na kuhakikisha wanatanua wigo hadi kufikia chuo kikuu.

## HABARI KITAIFA

# Wabunge waichachamalia TPA



Catherine Ruge

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WABUNGE wamechukizwa na hatua ya Mamlaka ya Bandari (TPA) kushindwa kufunga mfumo thabiti wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) na kudai kwamba umeisababishia serikali kupata hasara kutokana na kukusanya mapato kiduchu.

Wamesema tangu mwaka 2010 hadi sasa ni miradi mitatu tu ya Tehama iliyotekelezwa kati ya tisa na kusababisha upotevu mkubwa wa mapato, licha ya makandarasi kulipwa Sh. bilioni 57.5 kutekeleza mifumo hiyo.

Wakichangia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), mwishoni mwa wiki kuhusu taarifa za ukaguzi za CAG kwa hesabu zilizokaguliwa za serikali na mashirika ya umma kwa mwaka 2018/19, wabunge hao walisema ni muda wa miaka mitano imepita, lakini TPA imeshindwa kutekeleza agizo la kufunga mifumo ya Tehama.

Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Catherine Ruge, alisema hoja ya mifumo ya kielektroniki TPA imekuwa ikipigiwa kelele kwa muda wa miaka mitano, lakini wameshindwa kutekeleza.

Alisema TPA imeshindwa kutekeleza ukusanyaji wa mapato, kuhakikisha taasisi mbalimbali kama Benki, Mamlaka ya Mapato (TRA) na bandari kavu kusomana.

"Kuna mfumo unaitwa ERP ulianza kutekelezwa miaka mitano iliyopita, lakini mkandarasi ameendelea kulipwa na mpaka sasa mfumo haujakamilika, kuna mfumo mwingine unaitwa POS unatekelezwa na wafanyakazi wa ndani wa bandari kwa kushirikiana na mshauri elekezi ambaye hadi sasa anaendelea kulipwa kinyume na utaratibu na makubalinao ya mkataba," alisema Ruge.

Alisema TPA imeshalipa Sh. bilioni 57.5 kwa ajili ya kutekeleza mifumo ya Tehema ambayo haijakamilika na haifanyi kazi kwa ufanisi, na serikali kuendelea kupata hasara mwaka hadi mwaka.

"Mimi ninaamini kuna watu wananufaika kwa kutokukamilika kwa mifumo hii, ndiyo maana wanachelewesha isikamilike kwa wakati," alisema Ruge.

Mbunge huyo alisema TPA kumekuwa na tatizo katika menejimenti la muda mrefu ambalo halijapatiwa ufumbuzi.

Ruge alisema tangu mwaka 2017 kuna idara au vitengo TPA vimekuwa vikivunjwa kwa makusudi kwa manufaa ya mtu ili visitekeleze malengo yake.

Akitolea mfano, Ruge alisema: "Kwa mfano Idara ya Tehama tangu mwaka 2017 imekuwa na mkuu wa idara kila mwaka, ambaye anafukuzwa au kuacha kazi au kuhamishwa, wa mwisho ameacha kazi miezi iliyopita kutokana na kutoelewana na uongozi."

Aliongeza: "Idara ya ukaguzi wa ndani tangu mwaka 2017 imekuwa na wakuu wa idara kila mwaka. Mwaka 2019 kulikuwa na Head of Internal Auditor (Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani) ambaye ana elimu ya PhD, alihamishwa kutoka makao makuu kwenda Mpanda kuwa Desk Officer".

"Hivi tunavyozungumza idara ya ukaguzi wa ndani, idara nzima imesimamishwa kazi, watu zaidi ya 13 wamesimishwa kazi sababu ili kupisha ukaguzi wa ndani wa CAG. Kuna wakati ilionekana timu ya Finance ilienda Bandari ya Kigoma na Mtwara kufanya ukaguzi wakati kazi hiyo ni ya Mkaguzi wa Ndani. Serikali inapaswa kuweka jicho la karibu bandarini."

Ruge alisema Wakala wa Serikali apewe kazi ya kukamilisha mifumo ya Tehama TPA ili serikali isiendelee kupata hasara.

Mbunge wa Tanga Mjini (CCM), Mussa Mbarouk, alisema mfumo wa uendeshaji bandarini kwa njia ya kielektroniki haujakamilika, kwa miaka minne TPA wanapoitwa katika Kamati ya PAC wamekuwa wakipiga chenga.

"Mara wanasema mingine imekamilika, mingine haijakamilika, lakini naomba kusema kuwa kutokukamilika kwa mifumo hiyo ndiyo chanzo kikubwa cha upotevu wa mapato bandarini," alisema Mbarouk na kuongeza:

"Serikali ipaangalie sana bandarini, hapo ndipo lango kuu la biashara, kama hatuwezi kupadhibiti basi miaka nenda rudi tutaishia kuzisifu nchi zingine. Yawezekana viongozi wa TPA hawajui wajibu wao au wameweka maslahi yao mbele," alisema Mbarouk.

Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashidi Shangazi, alisema pamoja na kuongezeka kwa shehena bandarini, lakini mfumo wa ukusanyaji mapato bandarini hauko vizuri.

Alisema eneo la kusimika mifumo ya kielektroniki limechukua muda mrefu, na kwamba hata shughuli za ununuzi na mikataba halijakaa vizuri.

# Upandaji wa miche michikichi Oktoba

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema upandaji wa zao la michikichi utaanza rasmi Oktoba mwaka huu na kama kuna mtu mmoja mmoja au kikundi wanataka kulima chikichi, waandae mashamba yao na miche ya awali watapewa bure.

"Serikali imedhamiria tulime zao hili kwa wingi na tuwasaidie wakulima kwani tunatumia pesa nyingi sana kununua mafuta ya mawese kutoka nje. Tukilima kwa wingi tutajitosheleza na hatutaagiza mafuta kutoka nje."

Waziri Mkuu aliyasema hayo juzi baada ya kukagua kitalu cha miche ya michikichi cha Halmashauri ya Kigoma Ujiji pamoja na kitalu cha JKT Bulombora akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Kigoma.

Vile vile, amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia mstaafu, Emmanuel Maganga, ahakikishe JKT Bulombora wanapewa ardhi waliyoomba kwa ajili ya kupanua kilimo cha michikichi.

Waziri Mkuu alisema kwa sasa Tanzania haitaagiza mbegu za michikichi kutoka sehemu yoyote duniani, na badala yake itazalisha mbegu zake yenyewe. "Tayari tuna miche milioni 1.8 na wataalamu wetu wanaendelea kuzalisha."

"Michikichi Kigoma ndio uchumi, tunataka wakulima wengi walime zao hili na Kigoma ndio chanzo cha zao la michikichi, ndio iliyotoa chikichi kwenda nchi nyingine."

Waziri Mkuu alisema awali kituo cha utafiti wa zao hilo kilikuwa jijini Dar es Salaam, serikali ikaona haiwezekani na kuamua kukihamishia Kihuinga, mkoani Kigoma.

Alisema wataalamu walihamishiwa Kihinga na wameshazalisha zaidi ya miche milioni 1.8 na kazi iliyobaki ni kuwapa wananchi ili waweze kupanda kwenye mashamba yao.

Pia, Waziri Mkuu amewaagiza maofisa kilimo wawasaidie wakulima kulima zao hilo kitaalamu pamoja na wale wenye michikichi ya zamani jinsi ya kuitoa na kupanda michikichi mipya.

Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, Omar Mgumba, alimshukuru Waziri Mkuu kwa maelekezo yake ya kuagiza miche ya michikichi igawiwe bure kwa wananchi. "Tumetumia Sh. bilioni 10.8 kwa ajili ya zoezi hili, na hizi ni jitihada za Rais John Magufuli."

Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Faraji Kasibi, alisema wizara yao itaendelea kutekeleza majukumu yake hasa katika kuisimamia JKT katika maeneo ya kilimo, ujenzi na viwanda.

Awali, Brigedia Maganga, alisema wanaishukuru serikali kwa uamuzi wa kusimamia zao hilo ili kuhakikisha linafanya vizuri na kuzalisha mafuta ya mawese.


**ZANZIBAR INSURANCE CORPORATION**

**EMPLOYMENT OPPORTUNITIES**

Zanzibar Insurance Corporation was established on the 20th June, 1969 under the Public Enterprises Decree of 1966 legal Notice no.11 of 1969. It is now operating under the Public Investment Act No.4 of 2002. The Corporation is a Parastatal Organization owned by the Revolutionary Government of Zanzibar through the Ministry of Finance and Planning. Zanzibar Insurance Corporation is looking for a qualified candidate to fill the following vacancies:

| | |
|---|---|
| **Job Title:** | **Human resources Officer-(1 Post)** |
| **Report to:** | **Manager Human Resources and Administration** |
| **Duties station:** | **Dar es Salaam** |

Job Purpose
The Human Resources and Administrative Officer is responsible for all Administration issues in the Corporation

Duties and Responsibilities
(i) Manages and coordinates all Administrative activities in the Corporation.
(ii) Supervises the work of Secretaries, drivers, guards, Office attendants and Clerical staff and ensures that all staff cooperates closely.
(iii) Deals with administrative functions like Office management, transport, staff welfare etc.
(iv) In charge of registry staff and registry activities, clerical staff, preparation and maintenance of staff records and statistics, correspondences handing

Qualifications:
- Bachelor Degree in Human Resource or Public Administration from a recognized University
- Proficient training in relevant field will be an added advantage.
- Computer Literacy.

REMUNERATION
Remuneration will be according to Zanzibar Public Service scale and other terms and conditions of ZIC.

MODE OF APPLICATION
Application letters accompanied by a typed detailed CV, certified copies of Academic Certificates, Three Names of Referees, Current Postal Address, Phone Number, Email Address and two current Passport Size .ApplicationShould be addressed to:

**MANAGING DIRECTOR**
**ZANZIBAR INSURANCE CORPORATION**
**P.O. BOX 432**
**MAISARA - MPIRANI**
**ZANZIBAR**

**Deadline: 12/06/2020**

IMPORTANT NOTE:
i) Testimonials/provision results /statements of results are not accepted
ii) Employed applicants are required to channel their application letter through their employers
iii) Age 25-35 years

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari corona ni jukumu la mashabiki

**HATIMAYE** serikali imetangaza rasmi kuruhusu Ligi za Soka kurejea ikiwa ni baada ya kusimama kwa takriban miezi miwili na wiki kadhaa kutokana na kuibuka kwa mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19, ambavyo vinaendelea kuitesa dunia hadi sasa.

Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili, ambazo ni sehemu ya michezo iliyokuwa imesimama tangu Machi 17, mwaka huu, ndizo ambazo zimeruhusiwa kurejea, huku michezo mingine ikitakiwa kusubiri hadi hapo serikali itakapotangaza vinginevyo.

Hata hivyo, licha ya serikali kuruhusu ligi hizo tatu kurejea, imezitaka wizara husika; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusika katika kutoa muongozo wa namna watakavyochukua tahadhari ili kuepuka maambukizo.

Na tayari Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bodi ya Ligi (TPLB), ikishirikiana na wizara hizo imetoa mwongozo kwa kueleza kwamba mechi zote zitachezwa katika kituo kimoja cha Dar es Salaam kwa Ligi Kuu kwenye Uwanja wa Taifa, Uhuru na Azam Complex, wakati ile ya Ligi Daraja la Kwanza na la Pili ikichezwa jijini Mwanza katika Uwanja wa CCM Kirumba na Nyamagana, huku mashabiki watakaoruhusiwa kuingia wakiwa ni kati ya 10 hadi 20 na vikundi vya ngoma pekee.

Hiyo ni kutokana na kutambua ukweli kwamba virusi vya corona bado ni tishio na havijapata tiba wala chanjo, na hadi jana mchana duniani kote, tayari jumla ya watu 344,338 walishapoteza maisha kutoka 5,424,154 waopata maambukizo na kati yao 2,256,957 wakipona.

Kwa Tanzania pekee waliopoteza maisha ni 21 kutoka 509 waliokuwa wamepata maambukizo, lakini hadi serikali inafikia hatua ya kuruhusu ligi za soka kurejea, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli alieleza kuridhishwa na kasi ya wagonjwa kupona ambapo Mei 17, mwaka huu kwa mujibu wa takwimu alizozitoa wagonjwa waliokuwa wamebaki katika hospitali na vituo mbalimbali vya matibabu nchini walikuwa 144 tu.

Rais alisema hata wagonjwa hao waliosalia hospitalini wote walikuwa wanaendelea vizuri, jambo ambalo aliahidi kuruhusu michezo kuendelea endapo hali itazidi kuwa nzuri hatua ambayo aliitekeleza Mei 21, mwaka huu kwa kuruhusu ligi za soka kurejea.

Hata hivyo, kuruhusiwa kurejea kwa ligi hiyo huku mashabiki wakizuiwa kwenda viwanjani kushuhudia mubashara timu zao zikicheza, hii ina maana sasa watahamia katika kumbi mbalimbali za starehe, baa na vibanda umiza kushuhudia mechi hizo kama ambavyo husema mechi "haiwezi kunoga" ukiangalia mwenyewe nyumbani.

Wengi wanadai licha ya TFF na serikali kuzuia mashabiki kuingia viwanjani kushuhudia mechi hizo, lakini ni kazi kubwa kwao kuweza kuzuia watu kukusanyika katika kumbi za starehe na mabanda yanayoonyesha mpira maarufu kama vibanda umiza, jambo ambalo wanaona kuruhusiwa kurejea kwa ligi hiyo kutazidisha maambukizo.

Kwanza kabisa kama ambavyo katika nyakati tofauti Rais Magufuli amekuwa akisema Watanzania waendelee kuchapa kazi na kuchukua tahadhari zote kama inavyoelekezwa na wizara ya afya, tunaunga mkono kauli hiyo.


Pia tukumbuke mwenye jukumu la kuilinda afya yako ni wewe binafsi na si serikali wala TFF, hivyo ni wakati wa kila shabiki wa soka kuchukua tahadhari kama ambavyo wizara ya afya inaelekeza ili kujikinga na virusi vya corona.

Tunatambua kuna uwezekano mkubwa mashabiki wakaongezeka zaidi katika vibanda umiza kutokana na kuzuiwa kwenda viwanjani, lakini katika hili wanaomiliki mabanda hayo hawana budi kuchukua tahadhari zote kwa kuweka vitakasa mikono ikiwa ni pamoja na kutoruhusu misongamano mikubwa.

Ingawa tutambua pia itakuwa ni vigumu kwa wamiliki hao kuweza kuthibiti idadi ya watu kutokana na kutaka kupata maslahi makubwa, hivyo ni jukumu la kila mtu kutambua corona bado ipo, haijapata tiba wala chanjo na inaendelea kuua, hivyo kuchukua tahadhari ni muhimu na si suala la kupuuzia hata kidogo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Klabu ziache kulalamika, muhimu kumaliza msimu

**MIAKA** ya mwanzoni mwa '80, bendi ya Makassy Orchestra ilitoka na kibao chao kilichotokea kuwa maarufu kisemacho 'Binadamu Hatosheki'.

Baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo yanasema 'binadamu hatosheki, hata ukimpa nini milele hatoridhika. Ukimpa tano leo, kesho atataka kumi. Leo mvua ikinyesha atataka jua, kesho jua likiwaka hachoki kulalamika, atataka tena mvua.'

Nia yangu si kukumbushia nyimbo za zamani, ila nataka kueleza jinsi baadhi ya klabu ambazo zitaanza kulalamika baada ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi yake ya Ligi kuamua mechi zilizosalia za Ligi Kuu, Daraja la Kwanza Tanzania Bara na la Pili kuchezwa kwa vituo badala ya nyumbani na ugenini kama ilivyozoeleka.

Kupitia kwa waziri mwenye dhamana na michezo nchini, Dk. Harrison Mwakyembe, alitangaza kuwa Ligi Kuu Tanzania Bara itachezwa kwenye Kituo cha Dar es Salaam, Uwanja wa Taifa, Uhuru na Azam Complex.

Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara na la Pili itachezwa kwenye kituo cha Mwanza, kwenye viwanja vya CCM Kirumba na Nyamagana.

Hii ni baada ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli kuruhusu shughuli zote za michezo kuanza Juni Mosi, baada ya kusimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na janga la ugonjwa wa Covid-19, unaosababishwa na virusi vya corona. Tayari kwa mbali yameshaanza manung'uniko kutoka baadhi ya klabu.

Na kuanzia leo Jumatatu, kwenye vipindi mbalimbali vya michezo, tunaweza kusikia baadhi ya viongozi mbalimbali kila mmoja akiongea lake kuhusiana na hali hiyo.

Wapo ambao walianza kusikika wakitaka Ligi Kuu iendelee vile vile kwa mtindo wa nyumbani na ugenini, ili mradi tu kila timu ipate faida ya kucheza nyumbani, hasa kipindi hiki ambacho timu nyingi zinapigana kwenye janga la kushuka daraja.

Baadhi ya viongozi watakuja kulalamika kuwa kucheza kwenye kituo kimoja kwao ni gharama licha ya kwamba serikali imejitolea na kutenga pesa za kujikimu, lakini wapo watakaosema kuwa hazitoshi.

Kuna baadhi ya viongozi wanaweza kuanza kulalamikia ratiba baada ya kupangwa na kusema inazipendelea baadhi ya timu.

Kusema kweli kwa hali iliyofikia sasa ni lazima kila klabu na viongozi wake wakubaliane na hali halisi jinsi ilivyo kwani, hata haikutegemewa kama ligi hizo zitachezwa tena.

Najua kuwa baadhi ya viongozi wa klabu hawakutaka kabisa ligi zirudi na walitaka zivunjwe kwa sababu mbalimbali ambazo wenyewe walidhani kuwa wangenufaika nazo kwenye timu walizopo kwa kutoshuka daraja.

Hawa kwa kiasi kikubwa ndiyo wanaokuja na malalamiko, na wengine wataendelea pia kulalamika.

Ikumbukwe kuwa kila kinachofanywa sasa kinafanywa kwa dharura na si kama ilivyokuwa hapo mwanzo.

Lengo ni kuunusuru msimu huu wa ligi umalizike na wapatikane mabingwa halali wa kuiwakilisha nchi kwenye mechi za kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Kuliko kulaumulaumu, ilipaswa kuisifia na kuipongeza serikali na wizara zake mbili za Afya na Michezo, Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB) kwa kuhakikisha kuwa msimu huu hafutwi, na badala yake unamalizika ili maisha mengine yaendelee.

Kilichobaki sasa ni viongozi wa klabu zote kuzikusanya timu zao na kucheza mechi za ligi kwa mazingira haya haya mapya ambayo wamewekwa, badala ya kulalamika.

## HABARI KITAIFA

# Wapata ujauzito likizo ya corona

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WANAFUNZI wawili wanaosoma Shule ya Sekondari Kaselya Mwamala katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wamedaiwa kupewa ujauzito katika kipindi cha likizo ya kujikinga na maambukizo ya ya virusi vya corona.

Hayo yalibainishwa juzi na Ofisa Maendeleo Kata ya Mwamala, Sophia Philbert, wakati akitoa elimu ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, kwa wajumbe wa kamati ya mpango mkakati wa serikali wa kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (Mtakuwwa), kwa kushirikiana na Shirika la Agape.

Philbert ambaye pia ni Katibu wa Mtakuwwa Mwamala, alisema katika kipindi hiki ambacho wanafunzi bado wapo kwenye likizo ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona, wazazi wanapaswa kuzuia watoto wao wasizurure ovyo, ili kuwaepusha na athari ambazo watazipata ikiwamo kupewa ujauzito.

"Naombeni sana wajumbe wa kamati hii ya Mtakuwwa Mwamala muimarishe ulinzi wa mtoto na kutoa elimu kwa wazazi, wazuie watoto wao wasizurure ovyo mitaani hasa wa kike, bali wabaki majumbani na kujisomea, ili kuwaepusha na majanga mbalimbali ikiwamo kupewa ujauzito," alisema Philibert.

"Sasa hivi kuna wanafunzi wawili wa Shule ya Sekondari Kaselya hapa Mwamala wameshapewa ujauzito, mmoja kidato cha pili na mwingine kidato cha nne, jambo ambalo limesababisha kukatisha masomo yao na kuzima ndoto zao," aliongeza.

Aidha, alisema serikali inawatafuta watuhumiwa waliowapa ujauzito wanafunzi hao hawajulikani walipo, kwa kuwa walikimbia kusikojulikana baada ya kugundua wanatafutwa ili wakamatwe na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Naye Ofisa Tarafa ya Samuye, Ntarle Magese, alisema katika kipindi hiki cha likizo wana hofu ya kuwapo na mimba nyingi za wanafunzi, ambapo wameshajipanga kuwa pale shule zitakapofunguliwa watawapima ujauzito kwanza wanafunzi wote ili kujiridhisha kama wapo salama.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Shirika la Agape mkoani Shinyanga linalotetea haki za watoto, John Myola, alisema wameamua kuungana na serikali kutoa elimu ya ukatili katika kipindi hiki cha likizo ya corona, ili kuwakumbusha wazazi majukumu yao ya kumlinda mtoto wa kike pamoja na kutowaozesha ndoa za utotoni.




Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi (katikati), akimkabidhi vitambulisho vya ujasiriamali awamu ya pili 2020 kwa Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogolo, mkoani humo juzi, vilivyotolewa na Rais John Magufuli. Kushoto ni Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Angelina Lutambi. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**.

# Adaiwa kuuawa kwa wivu wa kimapenzi

**Na Stevie chindiye,**
TUNDURU

POLISI wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wanamshikilia Mussa Mohammed Yawani (57) kwa tuhuma za kumuua Raimu Rashid Mohammed (39).

Imeelezwa kwamba chanzo cha tukio hilo ni wivu wa kimapenzi.

Taarifa za tukio hilo zinaeleza kuwa marehemu Mohammed, mkazi wa Kijiji cha Naipingo wilayani Nachingwea alikumbwa na mkasa huo, akiwa kijijini Ligoma, wilayani Tunduru ambako alikwenda kwa ajili ya kutafuta maisha.

Walisema katika tukio hilo marehemu alikutwa akiwa chumbani kwa mtalaka wa mtuhumiwa.

Mtendaji wa Kijiji cha Ligoma, Jalasi Abdalah Jalasi, alidhibitisha kuwepo kwa tukio hilo na kwamba lilitokea usiku wa Mei 22, mwaka huu.

Jalasi alisema kuwa mtuhumiwa alienda nyumbani kwa mwanamke huyo na kupiga hodi akimuomba mtalaka wake atoke nje ili aongee na mtoto wao kwenye simu, lakini baada ya kufungua mlango mtuhumiwa aliingia kwa nguvu na kuanzisha ugomvi na marehemu.

Mganga aliyeufanyia uchunguzi mwili wa Mohammed, Dk. Stephen Hokororo, alisema chanzo cha kifo ni kutokwa na damu nyingi.

Alisema katika tukio hilo alibaini kuwapo kwa vidonda kwenye paji la uso, tumboni na shingoni vilivyo sababishwa na silaha.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo, na kwamba baada ya mtuhumiwa kutekeleza unyama huo, alikwenda kujisalimisha mwenyewe Polisi Mei 23, mwaka huu. baini kuwapo kwa upungufu wa sheria na miongozo inayowafanya wanawake kushindwa kushiriki kikamilifu katika uchaguzi na tayari tumewasilisha taarifa hii kwa vyombo vyenye mamlaka kama Bunge kwa ajili ya kufanya marekebisho," alisema.

## Bil. 4.7/- kutekeleza miradi ya elimu, afya

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, Anderson Msumba amesema, amepokea kiasi cha Sh. bilioni 4.7 kutoka kwenye mfuko wa maendeleo ya jamii kwa wawekezaji Mgodi wa Buzwagi na kuzielekeza kwenye miundombinu ya elimu na afya.

Pia alisema kuwa fedha hizo zimepatikana baada ya kupitisha sheria mpya ya madini ya mwaka 2017, kwamba fedha zote za maendeleo ya jamii zinazotengwa na wawekezaji zipitie kwenye halmashauri husika na kushirikiana kuibua miradi mbalimbali kwenye jamii.

Aidha, Msumba alisema kuwa kabla ya sheria hiyo fedha zilitajwa na kuonekana kwenye makaratasi zimetumika kuwapelekea wananchi huduma za maendeleo, lakini huduma hazionekani, na wananchi wanakiendelea kulalamika hasa kwenye elimu, afya na maji.

Msumba aliyabainisha hayo juzi wakati akizungumza na vyombo habari kabla ya kuanza kwa kikao cha Baraza la Madiwani cha halmashauri hiyo cha kujadili na kupitisha hoja za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), na kwamba alisema miradi mingi ilikuwa inatekelezwa na wawekezaji wenyewe.

"Mfano Kituo cha Afya Kata ya Mwendakulima kimejengwa na Mgodi wa Buzwagi kimegharimu dola za Marekani 700,000 na ambazo zinatosha kujenga Hospitali ya Wilaya na wananchi kupata huduma za matibabu," alisema Msumba.

Aliongeza: "Shule ya Msingi Mwime Kata ya Zongomela kuna nyumba za walimu zaidi ya tatu hadi nne zimejengwa pia na wawekezaji wetu wakubwa, na kila nyumba mmoja imegharimu kiasi cha shilingi milioni 300.

Hata hivyo, Msumba alisema kuwa tangu sheria hiyo mpya imeanza kufanyakazi, kwa mwaka Halmashauri ya Mji wa Kahama inapata kodi ya ushuru wa huduma ya pango kiasi cha shilingi bilioni 1, huku fedha za mfuko wa maendeleo ya jamii zikiwa Sh. bilioni 2.4.

Pia alisema mpaka sasa shule za msingi na sekondari katika halmashauri hiyo zinanufaika na fedha hizo kwa kujenga nyumba vya madarasa, masoko, vituo vya afya, barabara na wana mikakati ya kujenga bandari ili kuufanya Mji wa Kahama kuwa mji wa kibiashara kwa upande wa eneo la maziwa makuu Afrika.

HABARI KITAIFA




Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya Nyanza, wakiendelea na kazi ya kutengeneza mifereji ya maji ya mvua katika Barabara ya Kitunda na Kivule, Manispaa ya Ilala, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

# Mkuu wa shule, diwani wapewa kinyago ufaulu mdogo kidato 4

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

HALMASHAURI ya Chalinze Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, imemkabidhi Mkuu wa Shule ya Sekondari Vigwaza, Archad Kyokola, kinyago baada ya shule yake kufanya vibaya katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2019.

Alikabidhiwa kinyago hicho pamoja na Diwani wa Kata ya Vigwaza, Mohsin Bharwani, ili washirikiane na kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika mtihani ujao.

Kaimu Ofisa Elimu, Iren Rubega, alisema katika mitihani ya kitaifa iliyofanyika Novemba mwaka jana, halmashauri ilibahatika kuingiza shule tatu bora katika kumi bora za mkoa ambazo ni Chalinze, Talawanda na Shule ya Wasichana ya Mandera, ambapo Vigwaza ilikuwa ya mwisho kwenye ufaulu katika halmashauri hiyo.

Alisema shule zilizofanya vizuri zilipatiwa vyeti na iliyofanya vibaya ilikabidhiwa kinyago ili kila itakapokiona iongeze juhudi na kufanya vizuri.

Baada ya kukabidhiwa kinyago, mkuu huyo wa shule alisema sababu ya kushuka kiwango cha ufaulu ni pamoja na baadhi ya wanafunzi kuishi umbali mrefu na shule ilipo, lakini utoro pamoja na ushirikiano mdogo kutoka kwa wazazi.

Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, alisema kutolewa kwa kinyago hicho kutasaidia kuwakera walimu na kuwa na juhudi za kufaulu na kuongoza katika matokeo.

"Kama halmashauri inavyokereka na matokeo mabaya, mkuu wa shule naye amekabidhiwa kinyago ili kimkere ajisikie aibu na wafanye vizuri katika awamu inayo... wanatakiwa sasa mkuu wa shule na diwani washirikiane ili kuongeza ufaulu," alisema Ridhiwani.

Alisema hali hiyo itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu kwa halmashauri hiyo kimkoa na kitaifa.

# Mtandao walia kasi udhalilishaji nchini

**Na Joseph Mwendapole**

MTANDAO wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia (MKUKI), umeelezea kusikitishwa kwake na taarifa za ongezeko la unyanyasaji wa kijinsia nchini na duniani kama ilivyoripotiwa na Umoja wa Mataifa (UN).

Alisema hali hiyo imesababisha wanawake wengi 'kufungiwa' nyumbani pamoja na watesi wao, huku kukiwa na huduma hafifu za kusaidia waathirika kutokana na hofu na juhudi nyingi kuelekezwa kwenye mapambano dhidi ya mlipuko wa virusi vya corona.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Anna Kulaya, wakati akitoa tamko lililoandaliwa na mtandao huo kuhusu ukatili wa kijinsia wakati huu wa janga la corona.

Alisema mtandao huo unatambua umuhimu wa familia na nafasi ya wazazi katika kukuza amani ya familia, ustawi wa watoto, ulinzi na malezi hata kipindi cha hiki cha janga la corona na ndiyo sababu wamesikitishwa zaidi kusikia ongezeko la matukio ya vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia nchini Tanzania.

"Kwa pamoja, tumeamua kuandika taarifa hii ili kuweka bayana maoni yetu juu ya hali ya sasa ya mwenendo wa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia kipindi cha janga la corona, kutambua juhudi za serikali na wadau wake katika kufuta vitendo vya kikatili, kuelezea upungufu uliojitokeza na kutoa mapendekezo ya kisera," alisema Kulaya.

Alisema endapo mapendekezo hayo yatafanyiwa kazi na mamlaka husika pamoja na wananchi kwa ujumla yanaweza kusaidia kuondoa unyanyasaji wa kijinsia na kuendeleza haki za binadamu na kuhakikisha uwepo wa maisha bora kwa wanawake watoto na makundi mengine ya wanyonge.

Alisema kimataifa inaarifiwa kwamba wanawake na wasichana milioni 243 wenye umri kati ya miaka 15 na 49 wameshafanyiwa vitendo vya unyanyasaji wa kingono au wa kuumizwa miili yao ndani ya kipindi cha miezi 12 iliyopita, vitendo ambavyo wametendewa na wenzi wao wa karibu.

"Wakati Mkuki tunaendelea kukusanya takwimu rasmi juu ya hali halisi ya ukatili wa kijinsia (GBV) hususan unyanyasaji dhidi ya wanawake na wasichana, takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa matukio hayo yameongezeka. Kwa mfano, Ufaransa imeripoti kuongezeka kwa 30% ya ukatili wa majumbani tangu kuanza kwa tamko la kukaa ndani Machi mwaka huu, matukio kama hayo yameripotiwa pia huko Argentina, Cyprus na Singapore," alisema.

Alisema takwimu zilizowasilishwa na wanachama wa Mkuki na kikundi kazi namba 2 cha Mradi wa DDA ndani ya kipindi cha janga hili, inaonesha kwamba wasichana 176 na wavulana 76 wenye umri chini ya miaka nane wamekumbana na vitendo vya ukatili wa namna mbalimbali.

Alisema wanawake 474 wenye umri kati ya miaka 18 na 49 wamekumbana na vitendo vya kunyanyaswa kingono na kujeruhiwa miili yao kulinganisha na wanaume 144 ambao pia wamenyanyasika kijinsia.

# Shirika la Uturuki lasaidia chakula kwa kaya maskini

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

SHIRIKA la Ushirikiano la Uratibu la Uturuki (TIKA) limetoa msaada wa vyakula mbalimbali kwa kaya maskini Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani.

Kaya 150 zilinufaika na msaada huo uliotolewa mwishoni mwa wiki katika vijiji vya Kiparang'anda, Kitonga na Tengelea.

Akizungumza wakati akimkabidhi kwa Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filbato Sanga, ofisa wa Tika, Asca Sagwa, alisema wamekuwa na utaratibu wa kufuturisha kila mwaka katika misikiti mbalimbali.

Asca alisema, kutokana na ugonjwa wa corona, wanashindwa kufanya hivyo kwa mwaka huu, hivyo kuamua kutoa futari na chakula kwa kaya hizo.

"Tumeamua kuleta msaada huu katika wilaya ili wao watuelekeze pakupeleka baada ya kushindwa kufuturisha msikitini kama tulivyokuwa tunafanya awali, tumefanikiwa kuwafikia walengwa na hatutaamishia hapa, tutaendelea kusaidia kadri tutakavyoweza," alisema Asca.

Mratibu wa zoezi hilo, Rahma Mwita, alilishukuru shirika hilo kwa kukubali kufika katika wilaya hiyo na kutoa msaada huo, huku akiahidi kuendelea kushirikiana na wilaya hiyo atakapopata wadau wengine watakaosaidia wananchi katika nyanja yoyote.

Sanga alilishukuru shirika hilo, huku akisema familia zilizolengwa zitakazonufaika na msaada huo kwani ulifika wakati mwafaka.

Hanisi Sabili, mmoja wa wanufaika wa msaada huo, alisema vyakula walivyopatiwa vitawasaidia na familia zao.

Naye Fatuma Ally wa Kijiji Cha Kiparang'anda, alishukuru Shirika hilo pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambao wameainisha kaya zilizonufaika na msaada huo.

Msaada uliotolewa na Tika ni pamoja na tambi, chumvi 150, mchele kilo 450 mafuta lita 300, maharagwe na unga kilo 300 ambazo waligawiwa kaya maskini 150.

Kaya hizo zilizopatiwa msaada ni kati ziliziko kwenye mpango wa Tasaf katika Wilaya ya Mkuranga.

# Mkuranga yajipanga kukarabati barabara

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

SERIKALI imesema, imejipanga kurekebisha miundombinu ya barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, ambayo imeharibiwa na mvua.

Mvua hizo zimesababisha athari katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filbeto Sanga, wakati akizungumza na wakuu wa idara, wananchi na madiwani katika kikao cha Baraza la Madiwani.

Alisema mvua zinazoendelea kunyesha maeneo mbalimbali ikiwamo Mkuranga, zimeharibu miundombinu mbalimbali ikiwamo barabara.

"Kutokana na mvua kunyesha na kuharibu miundombinu ya barabara, serikali imepanga kurekebisha barabara za Mkuranga ambazo zimeharibika na mvua," alisema.

Pia Sanga aliwata madiwani kuendelea kushirikiana na wananchi katika kuwaletea maendeleo.

Alisema kwa kuwa Baraza la Madiwani halijavunjwa, waendelee kuwatumikia wananchi.

Aliongeza kuwa madiwani waendelee kuwaelimisha wananchi juu ya kuchukua tahadhari dhidi ya kujikinga na maambukizo ya corona.

"Pamoja na kutolewa elimu na serikali kupitia vyombo mbalimbali vya habari, madiwani pia mwendelee kuwaelimisha wananchi kuchukua tahadhari ikiwamo kunawa mikono kwa maji tiririka bila kusahau kuvaa barakoa."



Wafanyabiashara wa kuku wa kienyeji, wakiwa wamebeba tenga lenye kitoweo hicho, katika Soko la Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. Kuku mmoja aliuzwa kwa bei ya 17,000/- mpaka 25,000/- kulingana na uzito wake**. PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Wapewa angalizo kutouza chakula chote kuepuka njaa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa mazao ya biashara na chakula katika Halmashauri za Msalala, Kahama mjini na Msalala mkoani Shinyanga, wametakiwa kutouza mazao yao yote yaliyopatikana katika msimu huu ili kujilinda na janga la njaa ambalo linaweza kutokea.

Mazao hayo ni mpunga, mahindi, maharagwe, dengu na kwa mwaka huu wakulima wa Halmashauri za Msalala, Ushetu na Kahama Mjini wamepata mazao mengi ukilinganisha na msimu uliopita, lakini wengi wao wameanza kuuza mazao hayo.

Zainabu Telack, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, aliyabainisha hayo jana katika kikao maalumu cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri ya Mji wa Kahama cha kujadili na kupitisha hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali (CAG), alisema msimu huu wakulima wamepata mvua ya kutosha na kulima mazao mengi ya chakula na biashara.

Alisema kuwa, wakulima wa Halmashauri za Msalala, Ushetu na Kahama Mjini, wanatakiwa kuuza mazao ya chakula kwa uchache na kuhakikisha chakula kinabaki kingi ndani ya familia, kwani hakuna anayetambua msimu ujao kutakuwa na wingi wa upatikanaji wa mazao hayo.

"Hivi karibuni wakati Rais John Magufuli anatoka Chato tulipita nae na tukaona majaruba mengi yamejaa mpunga wa kutosha...hatutegemei kuona mkoa wetu tunakuwa na janga la njaa, hivyo uzeni mazao yenu kwa uchache na mhakikishe mnakuwa na chakula ndani," alisema Tellack, aliwataka madiwani wa halmashauri hiyo, kuhakikisha wanawasimamia wakulima wao kwenye maeneo yao ya utawala, kuhakikisha wakulima hawauzi mazao yote yaliyopatikana na kutunza chakula cha msimu huu na mwaka kesho.

Aidha, Tellack alimpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, kwa kupata hati safi na kwa mkoa mzima ambapo Halmashauri sita zilizopo zimepata hati safi kutokana na ushirikiano uliopo kati ya ofisi ya wakurugenzi na wataalamu.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa Albet Msovela, aliitaka Ofisi ya Mkurugenzi na wataalamu kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kuendelea kujibu hoja zilizopo na kupungua kutoka hoja 25 hadi hoja sita.

# Wenye ulemavu wakumbukwa vifaa corona

**Na Beatrice Philemon**

TAASISI ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kwa kushirikiana na umoja wa Watanzania waliosoma Australia (TAAA) chini ya udhamini wa Serikali ya Australia, wamekabidhi vifaa vya kuoshea mikono kwa watu waishio na ulemavu (PWD) vyenye thamani ya 7,900,000/-.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa NIMR, Prof. Yunus Mgaya, wakati wa makabidhiano ya vifaa hivyo.

Alisema vifaa hivyo vilikabidhiwa kwa Meya wa Ilala, Omary Kumbilamoto, kwa ajili ya watu waishio na ulemavu mkoa wa Dar es Salaam kwa ajili ya kupambana na maambukizo ya Covid-19.

Vifaa vilivyokabidhiwa ni pamoja na mashine nne za kuoshea mikono, kati ya mashine hizo, mashine tatu ni za kutumia pumpu ya mguu au mkono na moja inaendeshwa kwa kutumia umeme, lita 50 za sabuni ya maji, lita 20 za vitakasa mikono (sanitizers ), na vifaa vyote vimetengenezwa nchini kwa msaada wa Serikali ya Australia.

"Ninafahamu kwamba kuna wenzetu waliotangulia kuliona kundi hili la watu waishio na ulemavu katika sehemu mblimbali za nchi yetu na kuwasaidia kwa kupitia tukio hili, tunaamini tumeongeza na kuonyesha umuhimu wa kusaidia kundi hili ili waweze kukabiliana na Covid-19," alisema.

Alisema kwa kulitambua tatizo la Covid-19, NIMR kwa kushirikiana na TAAA chini ya udhamini wa Serikali ya Australia waliamua kubuni nyenzo za kuoshea mikono ambazo zinawapa urahisi wa kuzitumia watu waishio na ulemavu.

Ubunifu huo ulifanyiwa kazi na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mashine hizo ni matokeo ya muungano wa dhana na utekelezaji wa ubunifu huo.

Alitoa wito kwa taasisi nyingine, kampuni na watu binafsi kuendelea kujitolea katika kuhakikisha kuwa watu waishio na ulemavu wanasaidiwa ili waweze kuendelea kutoa mchango wao katika maendeleo ya nchi yetu.

Rais wa TAAA, Dk. Charles Makasi, alisema kutokana na rasilimali za wataalamu zilizopo kwenye TAAA, umoja huu hupenda kujenga uwezo, kutoa ushauri na ikiwezekana kushirikiana na taasisi zingine katika kuleta maendeleo.

"Lengo kubwa la TAAA ni kurudisha nyumbani ujuzi tulioupata masomoni ili kuchangia katika kuleta maendeleo ya nchi yetu," alisema.

## HABARI KITAIFA




Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Anna Kulaya (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, wakati akitoa tamko lililoandaliwa na Mtandao wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia (MKUKI), kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa corona. Wengine ni wanachama wa Mkuki, Janeth Mawinza (kulia) na Israel Ilunde. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**.

# Wanafunzi sayansi wapewa fursa elimu ya bure kiwandani

**Na Boniface Gideon,** TANGA

MWEKEZAJI wa gesi aina ya Oxygen na Nitrogen mkoani hapa, Mohamed Sayid, ameiomba serikali pamoja na wamiliki wa taasisi za elimu nchini kuwapeleka wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi kwenda kujifunza kwa vitendo kiwandani kwake kwa kuwa hatawatoza gharama yoyote.

Akizungumza na wanahabari kiwandani hapo, Sayid alisema licha ya kiwanda chake ni kipya, lakini yuko tayari kupokea wanafunzi wa masomo ya sayansi.

"Naiomba serikali pamoja na taasisi mbalimbali za elimu nchini hususani wanafunzi wa kuanzia sekondari na vyuo wawalete hapa bure wajifunze kwa vitendo, mwanafunzi wa sekondari shuleni anajifunza matumizi ya gesi mbalimbali, lakini hapa atakuja kujifunza kwa vitendo na atajionea namna inavyoandaliwa," alisema Sayid.

Alisema endapo wanafunzi wa masomo ya sayansi watakwenda kiwandani hapo na kujionea matumizi ya kisayansi yanayofanyika kiwandani hapo, itawahamasisha. "Wakija hapa wanafunzi wakiona tu itasaidia sana kuwaongezea nguvu na ari ya kuendelea kusoma masomo ya sayansi," alisema Sayid.

Aliongeza kuwa kwa sasa yupo katika hatua ya upanuzi wa kiwanda hicho. "Tunaendelea kukipanua kiwanda hiki kuna aina mbalimbali za gesi pamoja utengenezaji wa mabati ya kupaulia nyumba tutaanza kuzalisha hapo mbeleni na hii itawasaidia sana wanafunzi kuja kujifunza hususani kuanzia mwakani," alisema Sayid.

Alisema changamoto wanazokabiliana hivi sasa katika uzalishaji wa gesi ni ukosefu wa soko. "Unajua hiki kiwanda bado ni kichanga hivyo bado tuna matatizo ya soko, wateja wetu wakubwa kwa sasa ni Hospitali ya Rufani Mkoa wa Tanga 'Bombo', Simba Cement na Tanga Fresh, hivyo niwaombe wananchi na wahandisi na wamiliki wa viwanda mkoani humo na Tanzania kwa ujumla waache kwenda kununua hizi gesi nje ya nchi kwa sasa inapatikana Tanga," alisema.

# PDF, Unicef kuboresha afya, maji kwa mil.120/-

**Na Friday Simbaya,** NJOMBE

SHIRIKA la Maendeleo ya Watu PDF, limesaini mkataba na Shirika la Watoto Duniani (UNICEF) wa Sh. milioni 120 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya, maji, na usafi wa mazingira kwenye vituo vya kupambana na ugonjwa wa corona Njombe.

Akiongea na Nipashe jana Mkurugenzi Mtendaji wa PDF, Ndaisaba Ruhoro, alisema kuwa kazi hii inatarajiwa kutekelezwa ndani ya miezi mitatu katika vituo 4 vilivyotengwa kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa watu wanaoshukiwa kuwa na maambukizo ya virusi vya corona.

Alisema kuwa mradi huo utasaidia upatikanaji wa huduma ya maji, vifaa vya usafi na vitakasa mikono pamoja na usafi wa mazingira. PDF inatarajia kununua vifaa kutoka kwa wazalishaji wa hapa hapa nchini kama inavyo elekezwa na mamlaka za nchi.

"Hii itasaidia kuboresha huduma katika vituo hivyo pamoja na kupunguza hatari ya maambukizo kutoka kwa mtu kwenda kwa mtu mwingine," aliongeza Mkurugenzi Mtendaji wa PDF, Ndaisaba Ruhoro.

# Agizo wiki 1 kukamilisha ujenzi nyumba za walimu

**Na Jumbe Ismailly,** ITIGI

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni, mkoani Singida ametoa wiki moja kwa Idara ya Elimu Msingi katika halmashauri hiyo kuhakikisha inakamilisha ujenzi wa nyumba mbili za walimu katika shule za msingi Mkajenga na Mahinya.

Mwenyekiti huyo, Ally Minja, alitoa agizo hilo wakati wa kufunga mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo uliofanyika hivi karibuni katika ukumbi wa mikutano wa halmashauri hiyo.

"Lakini tumesisitiza masuala ya matumizi ya fedha ambazo tumeletewa na serikali kwa ajili ya miradi, kwanza miradi ya ujenzi wa umaliziaji wa nyumba mbili za walimu wa shule za msingi Mkajenga pamoja na Shule ya Msingi Mahinya," alifafanua Minja.

Minja hata hivyo alitumia wasaa huo kuwaagiza madiwani kwenda kupambana kwenye maeneo yao kwa kipindi cha wiki moja, na kuahidi kuwa naye atakwenda kuwasaidia kwa siku moja moja kwenye hayo majengo ili angalau fedha walizopewa waweze kuzitumia na kuzimaliza ili waweze kuomba nyingine.

Katika hatua nyingine, halmashauri hiyo imepokea jumla ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuboresha Kituo cha Afya cha Rungwa, na kwamba wananchi wameanza kujitolea nguvukazi kwa kuchota maji, kurundika mchanga na ufyatuaji wa matofali unatarajia kuanza hivi karibuni.

Alifafanua kwamba licha ya kupokea Sh. milioni 175 kwa ajili ya usafi wa mazingira za kujenga matundu ya vyoo ambazo mpaka sasa ni hazijaanza kutumika kutokana na kutopatiwa mwongozo wa jinsi ya kuzitumia fedha hizo.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, shule saba za msingi ndizo zilizopatiwa fedha hizo na kwamba endapo zitatumika kwenye matundu ya vyoo, shule hizo zitapata matundu ya vyoo bora vitakavyosaidia afya za watoto kuboreka.

Nipashe
Spotika



WANASOKA WA5 WA THAMANI ZAIDI 2010 DHIDI YA WA 2020 UK. 12&13

# 11 NA JEZI YA HISPANIA NJE YA BARCA, MADRID



DE-GEA

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid na Barcelona zimetawala soka la Hispania tangu kuanzishwa kwa ligi yake. Kiukweli, msimu wa kwanza wa LaLiga mwaka 1929 ulishuhudiwa timu zote mbili zikiwa juu.

Kumekuwa na klabu nyingine ambazo zimekuwa zikifanya vizuri, lakini pambano la timu hizi mbili limekuwa maarufu zaidi na kupewa jina la Clásico.

Lakini pamoja na yote, kumekuwa na wachezaji wa daraja la juu wenye vipaji vya ukweli wa nchini Hispania ambao hawajawahi kuzichezea klabu hizo mbili.

Kizazi cha dhahabu cha wachezaji wa Hispania kati ya mwaka 2008 na 2012, kuna wachezaj wake hawajawahi kuzitumikia timu hizo mbili.

**DAVID DE GEA**

Baada ya kukaa karibia miaka nane pale Atlético Madrid, klabu aliyojiunga nayo akiwa na umri wa miaka 13, lilikuwa jambo lisilotarajiwa wala kufikiriwa kama David de Gea asingejiunga na moja kati ya klabu hizo mbili, na Real wamekuwa wakijaribu kumsajili kwa miaka ya hivi karibuni.

**CÉSAR AZPILICUETA**

Azpilicueta ni mmoja kati ya wachezaji wanne tu aliyecheza katika kila dakika kwenye Ligi Kuu ya England. Azpilicueta tangu kutua kwake pale Chelsea amekuwa na kiwango kisichoshuka na amekosa mechi nne tu za Ligi Kuu kwa kipindi cha misimu mitano iliyopita.

**MLINZI - JUANMA LÓPEZ**

Mzaliwa huyu wa Madrid, Super López ametumia muda wake wote akiwa pale Atlético, akishinda taji lake la kwanza la ligi mwaka 1996 pamoja na Kombe la Mfalme [Copa del Rey].

**ANDONI GOIKOETXEA**

Andoni Goikoetxea au, 'muuaji wa Bilbao', kwa kipindi chake chote yeye alitamba kwenye klabu ya Athletic Bilbao na anakumbukwa sana kwa faulo aliyowahi kumchezaji Diego Maradona wakati akicheza pale Barcelona. Alishinda taji la LaLiga miaka ya 1980.

**JOAN CAPDEVILA**

Huyu ni mshindi wa Kombe la Dunia mwaka 2010, licha ya klabu hizo mbili kumuwania kwa udi na uvumba, Joan Capdevila hakuwahi kuonyesha dalili yoyote ya kuvutiwa na timu hizo.

**JOAQUIN**

Katika umri wa miaka 38 na siku 140, Joaquin alikuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kufunga hat-trick kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga. Na bado anaendelea kutamba katika klabu yake ya Real Betis. Akiwa na rekodi ya kuwa mchezaji wa tatu kucheza mechi nyingi zaidi kwenye historia ya LaLiga akifikisha mechi 550.

**SANTI CAZORLA**

Arsène Wenger alimsifia sana kabla ya kumsajili Cazorla, aliwahi kunukuliwa akisema: "Ni raha kumuangalia akicheza. Inavutia namna anavyofanya mambo dimbani. Natumaini kila mchezaji kijana nchini England anamtazama yeye."

**RUBÉN BARAJA**

Rubén Baraja alishinda mataji mawili ya LaLiga na Kombe la Mfalme [Copa del Rey] na la Uefa kwa kipindi cha miaka 10 pale Valencia. Licha ya kuwa na uwezo mkubwa dimbani, lakini hakuwahi kuvaa jezi za klabu hizo mbili.

**DAVID SILVA**

Pamoja na Vincent Kompany na Sergio Agüero, David Silva ni mmoja wa wachezaji watatu kuwa sehemu ya kikosi cha Manchester City mara zote nne ilizotwaa taji la Ligi Kuu ya England.

**JUAN CARLOS VALERÓN**

Juan Carlos Valerón alicheza mechi zaidi ya 400 za LaLiga akiwa amepata kadi moja tu nyekundu. Kwa kipindi cha zaidi ya muongo mmoja imani yake ilikuwa kwa Deportivo La Coruña.

**FERNANDO TORRES**

Torres kwa kipindi cha misimu mitatu na Liverpool alifunga zaidi ya mabao 56 na alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia sana.

Lakini uhamisho wake wa kwenda Chelsea haukuwa na mafanikio makubwa, kwani kiwango chake kilishuka. Alikuwa kwenye kikosi cha Hispania kilichokuwa na mafanikio makubwa zaidi kati ya mwaka 2008 na 2012.

## ISIKUPITE

BEKI wa Kati wa Inter Club d'Escaldes, Ildefons Lima ambaye aliichezea timu ya Taifa ya Andorra kwa mara ya kwanza mwaka 1997. Ameendelea kuichezea kwa miaka 23 akiichezea mara 128, na licha ya umri wake wa miaka 40 alionao kwa sasa, bado yupo fiti kuitumikia na ndiye anayeshikilia rekodi ya dunia kwa kuitumikia timu ya taifa kwa muda mrefu zaidi kwa upande wa soka la wanaume.



## Extra Time

# WANASOKA WA5 WA THAMANI ZAIDI 2010 DHIDI YA WA 2020

**LONDON, England**

KUANZIA mwaka 2010 kumekuwa na matukio mengi zaidi kwa kipindi cha muongo mmoja yaliyotokea katika historia ya mpira wa miguu duniani. Mengi yamepita kwa miaka hii kumi. Wakati Lionel Messi na Cristiano Ronaldo wamebakia kuwa wachezaji wawili wa daraja la juu kabisa duniani, kumekuwa na mabadiliko mahali pengine kwenye mchezo huo, haswa kuhusu suala la soko la wachezaji.

Tumeshuhudia kuchomoza kwa klabu mbili - Manchester City na PSG, kutoka chini hadi kutamba Ulaya. Kwa upande mwingine, pia tumeona klabu kama Manchester United na AC Milan zikisuasua kuishi katika viwango vyao vya juu. Real Madrid imejipambanua yenyewe kuwa moja ya klabu yenye mafanikio makubwa zaidi Ulaya.

Lakini moja ya mabadiliko maarufu zaidi ni kuongezeka kwa bei ya wachezaji kwenye soko la uhamisho. Mwanzoni mwa muongo huu, ada ya milioni 50 kwa Fernando Torres ilitosha kuvunja rekodi ya uhamisho Uingereza. Leo, mtu atalazimika kutoa mara nne ya kiasi hicho kuvunja rekodi ya dunia. Ada ya PSG ya pauni milioni 198 kwa ajili ya Neymar labda ilikuwa kichocheo kikuu nyuma ya mfumuko huu wa bei. Lakini bila kujali sababu, ni wazi kuwa mchezaji mzuri sasa ni lazima atalipwa kiasi kikubwa zaidi tofauti na miaka kumi nyuma.

Ni nani walikuwa wachezaji watano wenye thamani zaidi duniani mwaka 2010, na wanalinganaje na wale wa sasa wa 2020? Ni wakati wa kujua...

**#5. Ricardo Kaká (Euro mil. 60) na Mohammed Salah (Euro mil. 120)**

Real Madrid iliilipa AC Milan euro milioni 67 wakati wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2009 kwa ajili ya kupata huduma ya kipaji cha Kaka wa Brazil. Wakati huo alikuwa na umri wa miaka 27, Kaka alitarajiwa kuwa kwenye kiwango cha juu kwa miaka mingi pale katika dimba la Santiago Bernabeu. Bahati mbaya mambo hayakwenda kama yalivyopangwa kwa kiungo huyo, alishindwa kuonyesha kiwango chake nchini Hispania.

Hata hivyo, Kaká bado kirahisi tu alikuwa mmoja wa wachezaji bora kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita, na hata thamani yake mara zote ilikuwa kubwa. Alistaafu Desemba mwaka 2017 - miezi michache baada ya Liverpool kulipa euro milioni 42 kwa ajili ya Mohammed Salah.

Salah aling'ara kwenye soka la England, akivunja rekodi ya Ligi Kuu katika msimu wake wa kwanza. Haikuchukua muda watu kusahau kiasi cha ada kilichotolewa kwa ajili ya kumrudisha tena England.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri amejiimarisha yeye mwenyewe na sasa thamani yake imepanda maradufu zaidi. Katika umri wa miaka 27, Salah anaendelea kuwa mmoja wa mawinga bora kabisa duniani, na haitashangaza kuona thamani yake ikipanda hadi euro milioni 120.

**#4. Andres Iniesta (Euro mil. 60) na Sadio Mane (Euro mil. 120)**

Katika umri wa miaka 26, Iniesta alikuwa mmoja wa wachezaji wa kuvutia zaidi duniani mwaka 2010. Kwa uhakika kabisa bei yake ilikuwa kubwa zaidi kama angeondoka Barcelona. Akifunga bao la ushindi kwenye fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2010 na thamani yake ilipanda zaidi tofauti na ilivyotarajiwa.

Iniesta pengine alikuwa mmoja wa viungo aliyekuwa akihitajika zaidi siku hizo, na kwa sababu mbalimbali. Sasa akiwa na umri wa miaka 36, Iniesta anaendelea kuwashangaza mashabiki wa Vissel Kobe nchini Japan.

Hata hivyo, inaeleweka wazi kwamba, patina wa Salah pale Liverpool, Sadio Mane anatengeneza zaidi vichwa vya habari kulikosa Iniesta.

Mane anacheza soka bora zaidi katika umri wake wa miaka 28, na mara kwa mara amekuwa akihusishwa na kutakiwa kule Real Madrid. Kama Salah, yeye ni mmoja wa viungo bora kabisa duniani, na wengi wanaamini Mane pengine ni bora zaidi kuliko raia huyo wa Misri.

Raia huyo wa Senegal ana kila kitu anachotakiwa kuwa nacho winga. Kiukweli hata kiasi cha euro milioni 120 kinaweza kisitoshe kwa Liverpool kumuachia aondoke.

**#3. Xavi (Euro mil. 65) na Neymar (Euro mil. 128)**

Ingawa Xavi tayari alikuwa akisherehekea umri wa miaka 30, mwanzoni mwa muongo huu, thamani yake ilikuwa ya juu.

Akiwa ametoka kwenye mafanikio makubwa katika michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2010, Xavi alikuwa mmoja wa viungo bora zaidi duniani wakati huo.

Kiasi cha euro milioni 65 kama ofa ya kumsajili Xavi kwa uhakika kabisa ingekataliwa na Barcelona. Xavi hata katika umri wa miaka 35, aliisaidia Barcelona kushinda mataji matatu - ingawa kwa msaada pia wa wachezaji wenzake kama Neymar Jr.

Mwanzoni mwa muongo, mmoja wa mchezaji kijana aliyekuwa kwenye kiwango cha juu zaidi ni Neymar wakati akicheza kule Santos. Hivyo, Barcelona wakaamua kulipa kiasi cha euro milioni 88.20 kwa ajili ya kumsajili Mbrazil huyo.

Baada ya kufurahia mafanikio kwa kubeba mataji mengi nchini Hispania, Neymar alihamia PSG kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222. Bado thamani ya Neymar ipo juu hadi sasa.

**#2. Cristiano Ronaldo (Euro mil. 90) na Raheem Sterling (Euro mil. 128)**

Kama kuna mmoja wa wachezaji ambaye kipaji chake bado kipo juu kwa kipindi chote cha mwaka 2010 na 2020, basi ni Cristiano Ronaldo.

Ingawa alikuwa katikati ya ukame wa kukosa Ballon d'Or kwa miaka minne, Ronaldo alijiimarisha kwenye ufungaji wa mabao. Alikuwa akifunga 'hat-trick' karibia kila wiki. Kiasi cha euro milioni 90 ndio pekee kingekubaliwa na Real Madrid ingawa wao walilipa zaidi ya kiasi hicho kumsajili kutoka Manchester United mwaka 2009.

Los Blancos hao walitengeneza faida baada ya kumuuza kwa Juventus kwa kiasi cha euro milioni 100. Kwa mchezaji kuendelewa kuwa katika kiwango kile kile kwa kipindi cha miaka kumi si jambo la mchezo.

Raheem Sterling amefuata nyayo za Ronaldo. Ametoka kuwa winga na kuwa mfungaji wa mabao kama ilivyo kwa Ronaldo.

Katika soka, wafungaji mabao wanathamani kubwa zaidi kuliko mchezaji yeyote, kwani ndio wanaotengeneza ushindi kwenye mechi. Hivyo si jambo la kushangaza kuona thamani ya Sterling ikipaa kwa haraka.

Muingereza huyu ni mchezaji aliyekamilika, kwa chenga, kufunga na kutoa pasi za mwisho. Ana miaka 25, kama ilivyokuwa kwa Mreno huyo kwa mwaka 2010, na kama ataendelea kuwa kwenye kiwango cha juu kama Ronaldo, Sterling atastaafu kama mmoja wa wachezaji bora zaidi wa kizazi hiki.

**#1. Lionel Messi (Euro mil. 100) na Kylian Mbappe (Euro mil. 180)**

Nyuma mwaka 2010, Lionel Messi aliyekuwa na umri wa miaka 22, alikuwa mchezaji wa kwanza kufikia thamani ya euro milioni 100, akiwa ameshinda kwa mara ya kwanza Ballon d'Or mwaka 2009 na akaendelea kwa kushinda mara tatu Ballon d'Or. Hivyo unaweza kuona thamani yake ilivyoweza kupaa.

Anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi kuwahi kutokea duniani, Messi bei yake ni kubwa kiasi kwamba hauziki. Kiukweli Barcelona waliripotiwa kwamba wamekataa kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya Lionel Messi zaidi ya mara mbili. Wachezaji wengi wameibuka na kupotea kwa kipindi hiki cha muongo mmoja, lakini Messi ameendelea kuwa na kiwango kilekile. Licha ya umri wake wa miaka 32, thamani yake haijashuka chini ya euro milioni 100 kwa kipindi cha miaka 10 kati ya mwaka 2010 na 2020.

Akiwa ameweka rekodi ya kushinda mara sita Ballon d'Or mwaka 2019, Messi ameendelea kuonysha kuwa hana mpango wa kushuka kipaji.

Kylian Mbappe, ni kama Messi, alikuwa mchezaji wa kwanza kuwa na thamani ya euro milioni 200 katika umri wa miaka 21. Ameshinda mataji yote kwa misimu yake hadi sasa, ana Kombe la Dunia alililoshinda mwaka 2018.

Mbappe thamani yake kwa sasa ni kubwa zaidi na bado ana miaka mingi zaidi ya kuendelea kucheza na pengine ndiye anayeweza kuja kuvunja rekodi ya Messi na Ronaldo.



Cristiano Ronaldo

## Nukuu

"Lewy [Robert Lewandowski] yupo kwenye kiwango cha kuvutia, nafikiri anaweza kuifikia, amefunga mabao 26, na mechi nane zimebakia ili kuvunja rekodi ya Gerd Muller. Haitakuwa kazi rahisi, lakini ana ubora huo. Kama kuna mtu anaweza kuifikia basi ni yeye," **Kocha Mkuu wa Bayern Munich, Hansi Flick, akimtaka Lewandowski kuivunja rekodi ya mabao 40 kwa msimu inayoshikiliwa na Muller.**



"Nilishtuka wakati Louis [van Gaal] alipofukuzwa, kwa upande wangu, nilifurahia sana kufanya naye kazi, tulitakiwa kumbakisha kwa mwaka wa tatu. Tungekuwa imara zaidi," **Wayne Rooney katika Kitabu cha 'LVG - The Manager and the Total Person'.**



"Lakini nje ya uwezo wa Mungu, huwezi kuwa bora duniani kwa kuichezea PSG. Kwa hilo unatakiwa kwenda Real Madrid au Barcelona, kwenye timu ambayo unaweza kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Naamini PSG haitakuwa na uwezo wa kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa miaka mitatu au minne ijayo," **Mshambuliaji wa zamani wa Brazil, Giovane Elber akihoji maamuzi ya Neymar kujiunga na PSG.**





Wachezaji hawatapata sapoti ya mashabiki kama hawa Ligi Kuu itakaporejea mwezi ujao. **PICHA: MAKTABA**

# TIMU ZITAKUMBANA NA HILI LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

KAMA ilivyotangazwa, Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20, utaendelea tena hivi karibuni, baada ya kusimamishwa kwa takriban miezi miwili hivi kutokana na dunia kukumbwa na ugonjwa wa Covid-19, unaosababishwa na virusi vya corona.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, Alhamisi iliyopita, wakati akiapisha wateule wake kwenye Ikulu ya Chamwino Dodoma, pamoja na mambo mengine, alitangaza rasmi kurejesha shughuli za michezo kuanzia Juni Mosi mwaka huu.

Jioni yake, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, akatangaza kuwa ni ruhusa sasa kwa timu zote za mpira wa miguu kuanza mazoezi, ili ikifika Juni Mosi, basi angalau wachezaji wawe wameshafanya mazoezi ya kutosha na wako fiti.

Kesho yake siku ya Ijumaa, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, akatangaza utaratibu utakaotumika kwa ajili ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi Daraja la Kwanza na la Pili pia.

Ligi itachezwa sasa kwa mtindo wa vituo, badala ya nyumbani na ugenini kama ilivyo kawaida ili kumalizia msimu huu.

Ligi Kuu itachezwa kwenye kituo cha Dar es Salaam, katika Uwanja wa Taifa, Uhuru na Azam Complex, huku Daraja la Kwanza na la Pili zitachezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba na Nyamagana mjini Mwanza.

Pia serikali ikatangaza kutenga kiasi cha Sh. milioni 417 kwa ajili ya kuziwezesha timu zinazoshiriki ligi hizo nchini kumalizia msimu.

Ligi inarejea, ingawa kwa tahadhari kubwa kwani wachezaji, makocha, viongozi na waamuzi watapimwa joto, huku kukiwa na uwezekano wa kuingiza mashabiki 10 au 20 tu wenye ngoma, kwa ajili ya kuchangamsha wachezaji uwanjani.

Hii ina maana kuna vitu vitakosekana au kupungua kama ilivyokuwa kawaida. Staili hii itanufaisha na kudhoofisha baadhi ya timu. Zingine zinanufaika upande huu na upande mwingine zitaathirika.

**Simba na Yanga kucheza bila mashabiki**

Kwa mara ya kwanza klabu kongwe, kubwa na zenye mashabiki wengi zitacheza bila ya kuwa na mashabiki wake ambao huwa wanajazana uwanjani kila zinapocheza na kusafiri nazo kila zinakokwenda.

Wachezaji wa klabu hizo watakuwa 'wanamisi' zile kelele za kushangiliwa na kila kizuri kinachofanywa uwanjani kiasi cha kuwachanganya hata mashabiki wa timu pinzani.

Kisaikolojia hii itaziathiri sana klabu hizo ambazo sasa wachezaji wake watalazimika kucheza kama timu zisizo na mashabiki wengi baada ya kutotakiwa kuingia zaidi ya watu 10 au 20 hivi, kitu ambacho hazijazoea.

**Timu za mikoani kucheza ugenini**

Athari nyingine itakuwa kwa timu za mikoani ambazo zitakuwa ni kama zinacheza mechi zote zikiwa ugenini jijini Dar es Salaam. Na kibaya zaidi itaziathiri zaidi itakuwa kwa zile timu ambazo zitakuwa zikijipapatua kuepuka janga la kushuka daraja.

Nyingi ya timu hizi zimekuwa zikifanya kila njia ili kushinda mechi zake za nyumbani kwa mikakati ya ndani na nje ya uwanja, lakini kwa sasa haitokuwa hivyo tena. Zitakuwa ugenini Dar es Salaam, kwa hiyo kila timu itashinda kwa uwezo wake.

**Simba, Yanga, Azam na KMC kuwa nyumbani**

Timu za Simba, Yanga, Azam na KMC FC zenyewe zitakuwa na faida moja kubwa ya kucheza mechi zote zikiwa nyumbani.

Azam, ambayo uwanja wake wa Azam Complex umechaguliwa kuwa moja ya viwanja vitakavyotumika, imekuwa na kawaida ya kuutumia vema uwanja huo ambao hivi karibuni umefunguliwa baada ya kuwa kwenye matengenezo.

Simba, Yanga na KMC zenyewe zimekuwa hazishikiki zinapocheza kwenye viwanja vya Taifa na Uhuru ambavyo vimeteuliwa, hivyo timu za mikoani zitakuwa na kazi nzito kwa hilo.

**Timu za mikoani kutozomewa**

Faida kubwa kwa timu za mikoani ni kucheza bila presha ya mashabiki wa Simba na Yanga. Iwapo timu hizo zinazoitwa au kujiita ndogo zitatumia udhaifu huu, zinaweza kuzitesa sana timu za Simba na Yanga na kuwa kwenye wakati mgumu kwenye ligi hiyo.

Wachezaji wa timu za mikoani watacheza bila kuzomewa, au kupigiwa kelele nyingi za mashabiki wa timu hizo ambazo wakati mwingine huwachanganya sana.


Wakati wachezaji wa Simba na Yanga wakiathirika na kutokuwa na mashabiki wa kuwashangilia, wachezaji wa timu za mikoani watakuwa wakicheza kwa utulivu kwa sababu wao wameshazoea mara nyingi kucheza mechi kwenye viwanja ambayo mashabiki ni wa kuhesabu.

**Staili mpya za kushangilia**

Imeelezwa kwa sasa kuwa wachezaji mbali na kuwa wameambiwa wasiteme mate sana, ushangiliaji pia utakuwa ni wa tofauti na ule uliozoeleka wa kutokaribiana.

Ni kwamba kwa sasa bao likifungwa aina ya ushangiliaji itabadilika. Wachezaji hawatokaribiana. Ina maana staili zote ambazo mashabiki wa soka wanazijua zitabadilika. Inawezekana wachezaji wakaja na aina mpya ya ushangiliaji ya kukaa mbalimbali, lakini ikawa gumzo na kuvutia wengi, kwani kuna wachezaji wabunifu sana linapokuja suala hilo.

**JE, WAJUA?**



ARSENE Wenger amekiri ni mwenye furaha kuona Liverpool ikishindwa kuivunja rekodi aliyoiweka na Arsenal ya kumaliza msimu wa Ligi Kuu England 2003-2004 bila kupoteza mechi. Kikosi hicho cha Jurgen Klopp, Liverpool msimu huu kimecheza mechi 27 bila kupoteza kabla ya Februari kukubali kuangukia pua ya mabao 3-0 dhidi ya Watford.





# W'biashara wapewa unafuu vita corona

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

KAMPUNI ya Kupatana imeimarisha jukwaa lake la kuhakikisha Watanzania wanafanya biashara kwa kununua na kuuza bila mikusanyiko.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kupatana.com, Philip Ebbersten, alisema hatua hiyo ni kutoa fursa kutumia jukwaa hilo kufanya biashara wakati huu wa kudhibiti kasi ya maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Alisema malengo na mwelekeo wa Kupatana ni kuwa na wateja wenye mafanikio kwa kupatia suluhisho la kitaalamu ambalo litaongeza biashara hapa Tanzania.

"Kwa sasa tukiwa na janga hili la gonjwa la Covid-19 ni muhimu watu pamoja na biashara zao ziendelee kwa kuuza na kununua wakiwa mbali na mikusanyiko ili kujikinga na maambukizo ya corona, Kupatana ndio soko au mahali pekee pa kukupatia nafasi na fursa hiyo," alisema.

Ebbersten alisema ili kurahisisha ufanyaji biashara, Kupatana imeunganisha shughuli zake na huduma za M-Pesa.

"Kupatana pia inatangaza kwamba M-Pesa imeunganishwa kama njia mojawapo ya malipo katika jukwaa hili, kuanzia sasa, watumiaji wote wa M-Pesa watakuwa na uwezo wa moja kwa moja na kwa urahisi kujiunga na kutumia huduma ya Premium Ads, mteja anayelipia, utakuwa na uwezo wa kutumia huduma zote za matangazo ya Premium Ads. Hii inasaidia kujiwekea nafasi kubwa zaid ya kuuza bidhaa zako kwa haraka na kwa uhakika," alisema.

Aidha, Ebbersten alisema taasisi yake pia imepunguza ada ya matangazo na kutoka punguzo kwa asilimia 80.

"Vilevile, wakati ambapo tunazindua huduma za malipo kwa M-Pesa, pia tunapunguza ada kwa wateja wa matangazo ya Premium. Hii ni ofa maalum katika kipindi hiki cha ugonjwa wa Covid-19 ambayo inalenga kuhamasisha biashara ya masafa ili kuepuka misongamano. Tunatumaini kwa kufanya hivi tutashiriki katika kuzuia kuenea kwa virusi huku tukichangia katika kuendeleza biashara," alisema.

Alitoa rai kwa watu na wafanyabiashara wote kuwa na uwezo wa kulifikia soko kubwa zaidi hapa Tanzania kwa ada nafuu.

"Tunawapa watu na wafanyabiashara ambao hawana bajeti za matangazo jukwaa kubwa lenye mamilioni ya wateja wa uhakika ambao wanatafuta nini cha kununua," alisema.

# Hasunga awapa mbinu wakulima

Na Paul Mabeja, KONGWA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amewataka wakulima nchini kulima mazao yenye mahitaji makubwa katika soko la ndani na nje kama vile mboga, matunda na maua ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Hasunga, aliyasema hayo alipokuwa akikabidhi matrekta 8, kwa wakulima waliokopeshwa kupitia Mfuko wa Pembejeo nchini, (AGITF).

Alisema, taifa linahitaji sana bidhaa za mazao ya aina hiyo, hivyo ni fursa kwa wakulima kuhakikisha wanalima kwa wingi ili wajipatie fedha zitakazo wakwamua kiuchumi.

"Taifa tunahitaji mboga mboga, matunda pamoja na maua, hivyo basi wakulima wanatakiwa kulima sana mazao haya ili kukidhi soko la ndani na la nje kwani vitu hivyo vinahitajika sana sokoni," alisema Hasunga.

Aidha, alibainisha hivi sasa kilimo, kimekuwa na mchango mkubwa katika pato la taifa ambapo kwa takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa kimechangia zaidi ya Sh. bilioni 25.

Alisema serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kukikwamua kilimo nchini ikiwa ni pamoja na kuongeza fedha katika pembejeo.

"Mfuko wa pembejeo nchini katika mwaka huu umetoa kiasi cha Sh. bilioni 2 mpaka sasa na kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015, kulikuwa na matrekta 14,100 nchini mpaka sasa yamefikia 19,604, ambapo ni ongezeko la asilimia 38," alisema.

Alifafanua kuwa, utafiti unaonyesha kiasi cha ardhi nchini kilicholimwa kwa trekta ni asilimia 20, ambapo malengo ni kuhakikisha kuwa wanafika asilimia 50.

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Pembejeo nchini, (AGITF), Festo Mhimba, alisema kuwa matrekta hayo waliyokabidhi yana thamani ya Sh. milioni 284.

"Mpaka hivi sasa kwa mkoa wa Dodoma pekee tumeshakabidhi matrekta 203, ya mkopo kwa wakulima ukijumlisha pamoja na haya 8, ya leo," alisema Mhimba.

Akizungumzia mafanikio ya mfuko huo, alisema kuwa toka uanzishwe umepokea Sh. bilioni 35 na kutoa mikopo kwa wakulima mikopo 3,607, na kiasi cha Sh. bilioni 84, kimetumika.

"Kama mnavyoona tulipokea Sh. bilioni 35, lakini tumekopesha Sh. bilioni 84, hii ni kwa sababu tunakusanya na kutoa kwa wengi hivyo kiasi kinapanda," alisema Mhimba.

Alisema mikopo inayotolewa na mfuko wa pembejeo ni kwa ajili ya mkulima mmoja mmoja pamoja na wale walio katika vikundi.

"Mkulima anaweza kukopa, dhana za kilimo au pembejeo yoyote ile na mikopo yetu malipo yake ni kuanzia miaka miwili hadi mitano, na vigezo mkulima anatakiwa kupitia katika halmashauri yake ili itutuhibitishie," alifafanua.

Awali, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliutaka mfuko huo kuongeza nguvu katika kujitangaza ili wakulima watumie fursa ya mikopo inayotolewa kujikwamua kupitia kilimo.

"Niwapongeze sana kwa kazi nzuri ya kuunga mkono juhudi za serikali katika kuwakomboa wakulima kutoka katika kilimo cha kimaskini cha jembe la mkono, lakini mnatakiwa kujitangaza sana na siyo kukaa kimya kama mlivyo sasa hakuna anayejua uwepo wa fursa hii," alisema Ndugai.

Mmoja wa wakulima wanufaika wa mkopo huo kutoka Wilaya ya Kondoa, Hadija Ngoro, alisema utamsaidia kujikwamua kiuchumi kwani kilimo ndio mkombozi kwake na familia yake.



Mkulima Evelina Mwanika akianika juani ufuta ikiwa ni hatua za kukausha zao hilo, nje ya makazi yake, katika kijiji cha Chipogoro, wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma, juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kaya 10 zalala nje kisa kupisha shule, barabara

Na Paul Mabeja, DODOMA

KAYA zaidi ya 10, za mtaa wa Sulungai, Kata ya Ipagala jijini Dodoma zimekosa makazi na kulazimika kulala nje chini ya mti, baada ya nyumba zao kubomolewa kwa madai ya kupisha eneo la shule na upanuzi wa miundombinu ya barabara.

Wakizungumza, kwa nyakati tofauti katika eneo hilo, wakazi hao walidai kuwa wamevunjiwa nyumba zao bila kupewa notisi wala kulipwa fidia.

Kezia Mwashinga, alisema hivi sasa wanawakati mgumu kutoka na kulala nje pamoja na watoto wao baada ya nyumba zao kubomolewa na serikali ya kata hiyo.

Mwashinga, alisema kuwa mwaka 2002, waliombwa na uongozi wa kata hiyo, kutoa kiasi cha maeneo yao ili kujengwa kwa Shule ya Ipagala 'B'.

Alisema kuwa waliambiwa kuwa mara baada ya kutoa eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo, watalipwa fidia ya kupisha katika maeneo waliyotoa, lakini mpaka sasa hakuna walicholipwa.

"Tunashangaa sasa anakuja mwenyekiti wa mtaa wetu na kutuambia kuwa tunatakiwa kuondoa bati asubuhi na mchana wanakuja kubomoa, hali ambayo imetupa wakati mgumu hasa kuzingatia hivi sasa tunakabiliana na ugonjwa wa corona," alisema Mwashinga.

Naye Kimwaga Seif, alisema wanashangaa kubomolewa nyumba bila kupewa taarifa hali ambayo imesababisha baadhi ya vitu vyao kupotea.

"Sisi hatukatai serikali kufanya maboresho kama haya ila tunachoomba kupatiwa fidia kama ambavyo wenzetu wengine wamepatiwa kwanini sisi tutengwe katika hili?" Alihoji Seif.

Aidha, aliongeza kuwa wamekwenda katika ofisi ya mkurugenzi, pamoja na mkuu wa Wilaya ya Dodoma kutafuta msaada bila mafanikio.

"Tumekwenda juzi kwa mkuu wa wilaya akasema yeye hana taarifa za ubomoaji katika wilaya yake, hivyo barua tuliyo mpelekea hajaipata bado tukaondoka," alisema Seif.

Rose Lyoka, alisema wanaiomba serikali kupitia ofisi ya mkuu wa mkoa, kuingilia kati mgogoro huo kwani wao pia wanayo haki kama walivyo wananchi wengine.

"Sisi siyo wakimbizi pia tunayohaki ya kutendewa sawa kama walivyo fanyiwa wenzetu kwa kupatiwa fidia ya maeneo yetu sasa hivi tulivyo tutaenda wapi na corona hii, hata fedha hatuna za kusema tuende kupanga nyumba katika maeneo mengine," alisema Lyoka.

# RC awajibu wanaoibeza serikali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewataka wananchi mkoani humo, kuacha kuwajibu kwa maneno wanaoibeza serikali wakidai haijafanya maendeleo yoyote, badala yake wawaonyeshe miradi iliyotekelezwa.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazungumza na watumishi wa taasisi mbalimbali za serikali wakati wa uzinduzi wa kubomoa majengo ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo kwa ajili ya kujenga jengo jipya na la kisasa.

Chalamila alisema serikali imeidhinisha shilingi bilioni nne kwa ajili ya mradi huo na kwamba tayari fedha hizo zimeanza kutolewa.

Alisema mbali na mradi huo, serikali imetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya sekta ya afya, elimu pamoja na miundombinu ya barabara.

"Kuna watu wao kazi yao ni kutukana na kubeza, utasikia wakisema serikali haijafanya kitu katika mkoa wetu...muwajibu kwa kuwaonyesha kazi zilizofanyika ukiwamo ujenzi wa ofisi hii ambayo itakuwa ya mfano," alisema Chalamila.

Alimtaka mkandarasi anayejenga jengo hilo ambaye ni Wakala wa Majengo (TBA) pamoja na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya Must, kuhakikisha wanakamilisha ndani ya muda uliopangwa kwenye mkataba.

Kwa upande waka Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, alisema mchakato wa kuomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi hiyo ulianza mwaka 2012 wakati yeye alipokuwa anafika mkoani humo.

Alisema waliamua kuanza mchakato huo baada ya kuona majengo ya awali yamechakaa na baadhi yanatishia usalama wa watumishi waliokuwa wanatumia ofisi hiyo.

"Wakati huo tulikuwa hatupewi fedha kwa sababu ilianzishwa mikoa mipya na halmashauri mpya nyingi, hivyo serikali ilielekeza nguvu nyingi huko na sisi tuliambiwa tusubiri kwa sababu tulikuwa na mahali pa kukaa, hivyo kwa sasa tuna kila sababu ya kuishukuru serikali," alisema Mtunguja.

Alisema kwa sasa Mkuu wa Mkoa amehamishiwa kwa muda katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya na Mkuu wa Wilaya amehamishiwa katika Ofisi ya Ardhi ya Mkoa huo na hivyo wananchi wataendelea kupata huduma.

Meneja wa TBA wa Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Jafari Kiyoga, alisema wamejipanga kukamikisha jengo hilo ndani ya miezi 15 iliyopo kwenye mkataba na kwamba ikiwezekana watamaliza kabla ya muda huo.

Alisema watashirikiana na Must kuhakikisha jengo hilo linakamilika kwa viwango vilivyoainishwa kwenye michoro.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), akishuhudia moja ya majengo katika ofisi yake likibomolewa na katapila, juzi, ili kupisha ujenzi wa ofisi mpya ambayo inatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 15 kwa gharama ya Sh. bilioni 4. **PICHA: NEBART MSOKWA**.

# TFS yatoa angalizo ukataji miti ovyo

**Na Grace Mwakalinga**, MBEYA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Innocent Lupembe, amewatahadharisha wananchi kutojihusisha na vitendo vya kukata miti ovyo, ili kuepukana na athari za kimazingira zinazoweza kutokea kama vile jangwa.

Tahadhari hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Meneja Msaidizi wa TFS, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Innocent Lupembe, wakati akizungumza na Nipashe namna ambavyo wanakabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira.

Alisema shughuli za ukataji miti na uchomaji misitu moto kwenye hifadhi za misitu zimekuwa chanzo cha uharibifu wa mazingira na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

Alisema misitu ikitunzwa na kuhifadhiwa katika mazingira mazuri italeta manufaa katika jamii, lakini pia itakuwa urithi mzuri kwa vizazi vijavyo.

"Jukumu la kutunza na kuhifadhi misitu sio TFS pekee yake bali kila mwananchi anapaswa kulinda kwa kuhakikisha hakuna shughuli zozote za uvunaji, ukataji na uchomaji misitu zinafanyika taarifa zitolewe kwenye mamlaka kwa yeyote atakayekata miti ovyo ili hatua za kisheria zichukuliwe," alisema Lupembe.

Alisema katika kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania Kanda ya Mbeya kwa kushirikiana na wadau wengine, wameanzisha kampeni ya upandaji miti ambayo ni rafiki kwenye vyanzo vya maji kama vile mikuyu, miembe pori, migunga mipori 14.

Aliongeza kuwa Sera ya Misitu inahimiza ushirikishwa wa wananchi katika kutunza na kuhifadhi misitu kwa faida ya sasa na ya baadaye na kuongeza kuwa Sheria Namba ya 14 ya Mwaka 2002 inatoa mwongozo na taratibu kwa mwananchi kufuata anapohitaji kuvuna misitu.

Chifu wa Jiji la Mbeya, Rocket Mwashinga, aliwaomba TFS kuwaachia wao jukumu la kulinda misitu kwa sababu ni miongoni mwa majukumu waliyopewa tangu enzi.

Alisema wao ndio walikuwa wasimamizi wa misitu na waliweza kusimamia vizuri na kudhibiti uharibifu ukilinganisha na ilivyo sasa hivyo wakikabidhiwa jukumu hilo rasmi shughuli za uvamizi, ukataji na uchomaji misitu ovyo zitakwisha kwani wataweka sheria za kuwabana wananchi katika maeneo yao.

# Taarifa ukatili kwa wanawake, watoto zatakiwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wameaswa kutoa taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wanawake ili hatua stahiki zichukuliwe kwa wahusika kwa lengo la kukomesha vitendo hivyo kwenye jamii.

Meneja Programu wa Shirika lisilokuwa la kiserikali linalojihusisha na utoaji wa Elimu na msaada wa Kisheria (Mbepace), Laiki Ndagile, alitoa rai hiyo jana, na kueleza kuwa kundi la wanawake na watoto ndilo linaongoza kwa kufanyiwa vitendo vya ukatili viikiwamo vipigo visivyo vya kawaida na ubakaji.

Alisema licha ya wanawake na watoto kuwa waathirika wa vitendo vya ukatili bado jamii na watendewa wamekuwa waoga kuripoti vitendo hivyo kwenye vyombo vya sheria kwa sababu wanaofanya vitendo hivyo ni ndugu wa karibu.

"Kumekuwa na wogo kwa baadhi ya familia ndugu zao wamefanyiwa vitendo vya ukatili ikiwamo kubakwa au kulawitiwa wakiogopa kuharibu mahusiano dhidi ya watendewa na kuficha aibu, jambo ambalo ni kinyume na haki za binadamu nawaasa jamii tubadilike tusikubali kuvumilia hali hii alisema Ndagile," alisema.

Aliongeza kuwa Shirika la Mbepace limekuwa likitoa elimu ya msaada wa kisheria na kuwajengea uwezo maofisa watendaji, wenyeviti wa vijiji, walimu na wananchi kwenye wilaya za Kyela, Rungwe na Wilaya ya Mbeya.

Alisema elimu hiyo imesaidia kupunguza vitendo vya ukatili ambapo kipindi cha mwaka 2018/19 jumla ya kesi 528 ziliripotiwa kwenye shirika hilo.

"Tumejipanga kuzijengea uwezo taasisi za elimu husussani wanafunzi na kamati za wazazi ili washiriki kikamilifu kwenye ulinzi na haki za watoto kwenye wilaya tunazofanya nazo kazi," alisema Ndagile.

Mmoja wa wasaidizi wa kisheria kutoka Wilaya ya Kyela, Tatu Hussein, alisema wanafanya kazi kwenye mazingira magumu kwa sababu ya kukosa ushirikiano kutoka kwa viongozi wa vijiji wanapohitaji kutoa elimu.

Alisema baadhi ya viongozi huwachukulia wasaidizi wa kisheria kama adui kwa kuhofiwa kuingiliwa majukumu yao, hivyo aliiomba jamii kutambua umuhimu wao wa kuielimisha jamii kuhusiana na masuala mbalimbali ya sheria.

**Tumejipanga kuzijengea uwezo taasisi za elimu hususani wanafunzi na kamati za wazazi ili washiriki kikamilifu kwenye ulinzi na haki za watoto kwenye wilaya tunazofanya nazo kazi**





# Shein aeleza corona ilivyobadili mfungo Mwezi wa Ramadhani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Muhamed Shein, amesema kuwa maradhi ya corona yameathiri mwenendo wa baadhi ya taratibu za maisha na kuwafanya waumini wa dini ya Kiislamu kuitekeleze ibada ya funga mwaka huu katika mazingira maalum, tofauti na miaka iliyopita.

Amesema waumini hao wamelazimika kuziacha baadhi ya taratibu na utamaduni waliozoea kuufanya katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ikiwamo sala za jamaa za tarawehi na baadhi ya misikiti kufungwa.

Akitoa taarifa ya Iddi kwa vyombo vya habari, alisema mashindano ya Quran katika ngazi mbalimbali hayakuweza kufanyika na hakukuwa na mialiko ya futari kutokana na ugonjwa huo.

"Katika sikukuu ya Idd El Fitr ya mwaka huu, hatukuweza kukutana kwenye Baraza la Iddi, ambalo ni sehemu muhimu katika historia na utamaduni wa watu wa Zanzibar...kwa hivyo, pokeeni salamu zangu za Idd el Fitri Waislamu na wananchi wote," alisema Dk. Shein.

Alisema wakati wananchi wana furaha ya kusherehekea Sikukuu hii ya Eid el Fitri, ni muhimu kuzingatia kwamba bado nchi inakabiliwa na janga la corona.

Alisema maradhi hayo bado yapo, licha ya mafanikio ya kuridhisha yaliopatikana kutokana na jitihada zinazochukuliwa na serikali kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali.

"Tunafarijika kuona namna wananchi walivyokuwa imara katika kupambana na Covid-19 kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa wakati wote, mambo ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza kiwango cha maambukizo katika sehemu zote za Unguja na Pemba," alisema.

Dk. Shein alisema hadi Mei 20, mwaka huu, jumla ya wagonjwa 34 walioambukizwa maradhi hayo wanaendelea kupata matibabu katika vituo vitano tulivyoanzishwa, kutoka miongoni mwa idadi ya wagonjwa 134 iliyowahi kufikiwa Mei, Mosi 2020, ambapo wagonjwa wote hao wanaendelea vizuri.

Aliwataka wananchi kuendelee kujenga ujasiri na kuondoa hofu katika mapambano dhidi ya corona na kuendelee kufanya shughuli zao ili kuchangia katika kuimarisha uchumi, ambao umepata changamoto tangu yalipoingia maradhi hayo.

Aidha, alisema mafunzo mbalimbali yalipatikana katika ibada ya saumu, ikiwamo uaminifu na uadilifu na watu wengi walijitahidi katika kufanya haki na kuepuka kufanya vitendo viovu kwa ajili ya kupata radhi za Allah.

Aliongeza: "Tukumbuke kwamba tunaposhirikiana na serikali katika kuimarisha uchumi, kudhibiti mapato na kuzilinda rasilimali zetu mbalimbali, ni njia moja ya uaminifu na kufanya uadilifu."

Alieleza kuwa ni wajibu wa kila mtu kuyaendeleze mafunzo hayo waliyoyapata katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani popote na wakati wote katika maisha yao ya kila siku.

Akizungumzia mvua za masika zilizonyesha ambazo zimesababisha athari mbalimbali, alisema serikali inaendelea kufanya tathmini katika maeneo yote ya Unguja na Pemba yaliyoathirika, ili iweze kurejesha miundombinu iliyoharibika.

"Nawaagiza viongozi wa manispaa, mabaraza ya miji na halmashauri waongeze kasi katika kuimarisha usafi wa miji, ili tujikinge na maradhi ya milipuko, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunayadhibiti maradhi ya kipindupindu," alisema.

Alieleza kuwa mvua ni neema, hivyo wakulima waitumie neema hiyo kwa kuzidisha nguvu katika kilimo cha mazao mbalimbali pamoja na miti ya kudumu, ili tuimarishe mazingira pamoja na kuongeza upatikanaji wa chakula nchini.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kushoto), akiagana na baadhi ya viongozi wa dini na serikali Wilaya ya Kaskazini "B", baada ya kuhudhuria Swala ya Iddi El Fitri katika Msikiti wa Ijumaa wa Kiombamvua, Zanzibar, jana. **PICHA: OMPR – ZNZ**.

# Wazazi watakiwa ukaribu na watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), Ofisi ya Zanzibar, kimewataka wazazi kuwa karibu na watoto wao wakati wa kipindi hiki cha sikukuu ili kuwakinga na vitendo vya udhalilishaji.

Mkurugenzi wa Tamwa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema katika miaka iliyopita kipindi cha sikukuu huripotiwa kesi nyingi za udhalilishaji ambapo watoto waliopo chini ya umri wa miaka 18 hutoroshwa ama kubakwa.

"Pamoja na kuwapo kwa janga la (Covid -19) ambapo kwa mwaka huu sherehe za sikukuu hazitakuwapo, lakini tunaishauri jamii kuwadhibiti watoto ili kuepukana na vitendo hivi viovu ambapo wahalifu hupata fursa kutumia kipindi hiki cha kumalizika kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kufanya vitendo vyao viovu," alisema Dk. Mzuri.

Alieleza baadhi ya watoto huonekana wakizurura kwa wingi kwa kisingizio cha kwenda kupokea mkono wa Iddi, hivyo kuhatarisha ustawi wao ambapo wakati mwingine hugonga hata kwenye nyumba wasizokuwa na mahusiano nazo.

"Mara nyingine watoto hao huingia katika nyumba ambazo wanaishi wabakaji, hivyo kuwafanyia vitendo vibaya na pia hata mtaani hurubuniwa kwa kuambiwa wakapewe sikukuu yao."

Alisema ni vyema watoto kubakia chini ya uangalizi wa wazazi wao kwa wakati wote, ili kujilinda kutokana na wabakaji lakini dhidi ya maradhi ya corona.

Aidha, aliitaka jamii kuendelea kujilinda na maradhi ya corona na kufuata maelekeo ya wataalamu wa afya ili kuepukana na mambukizi ya ugonjwa huo.

# Waislamu washauriwa tathmini baada ya mfungo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAUMINI wa dini ya Kiislamu nchini wanapaswa kufanya tathmini ya kina baada ya kumalizika kwa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ili utekelezaji wa ibada zinazowajibikia katika safari yao ya ucha Mungu isiwe na dosari wala wasiwasi wa nafsi.

Hayo yameelezwa na Sheikh Ahmed Ashkina Ali wakati akitoa hotuba ya Ibada ya Sala ya Iddi El Fitri kwa waumini wa dini ya Kiislamu, ambayo pia ilihudhuriwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, katika Msikiti wa Ijumaa wa Kiomba Mvua Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja.

Sheikh Ashkina alisema Mwezi Mtukufu wa Ramadhan lazima uwe kigezo kizuri cha kuendelezwa katika miezi mengine inayofuata kwa vile kimeshibisha waumini kupata chakula ikiwamo usomaji wa kitabu Kitukufu cha Quran, kitendo kilichokwenda sambamba na masuala ya utoaji wa sadaka.

Alisema ucha Mungu wa moyo umekuwa ukisisitizwa kuwamo ndani ya vifua vya waumini utakaowawezesha kufikia daraja la juu inayomsafishia njia muumini kuwa na maisha mema kwenye safari yake ya milele.

Sheikh huyo aliwaeleza kwamba Iddi zote mbili, ile ya Fitri na Hajj ni siku maalum zilizowekwa na Mwenyezi Mungu kwa lengo la kuwapa furaha na bashasha waja wale bila ya kujali fukara, maskini au tajiri baada ya kukamilisha ibada zao.

Alisema Iddi hizo zina mnasaba maalum unaowapa waja kutafakari uwezo wa Muumba wao ambao unawajibisha kutekeleza vyema na kwa dhati ibada zao za kumcha Muumba huyo.

"Iddi El Fitri hufanyika baada ya kumalizika kwa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani wakati Iddi El Hajj inafanyika baada ya kumalizika kwa masiku kumi bora ndani ya mfunguo tatu," alisema.

Akizungumzia ugonjwa wa corona, aliwakumbusha waumini pamoja na wananchi kuendelea kuchukuwa tahadhari kubwa ya kujikinga na maradhi hayo.

Sala ya Iddi El Fitri zimefanyika katika misiki mbalimbali ya Ijumaa katika utaratibu wa kuzingatia kinga dhidi ya maradhi ya corona iliyosababisha kusitishwa kwa Sala ya Iddi kitaifa pamoja na Baraza la Iddi kwa mwaka huu.

HABARI PICHA

# MATUKIO YA SWALA YA EID EL FITRI KATIKA PICHA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akisalimiana na viongozi wa dini ya Kiislamu wa Mkoa wa Dodoma, alipowasili katika msikiti wa Gaddafi, kuhudhuria Swala ya Eid El Fitri, jijini humo jana. **PICHA: OWM**



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Ali Mohamed Shein, akitoa salamu za Eid El Fitri, baada ya kumalizika kwa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**



Baadhi ya kinamama wa dini ya Kiislamu Mkoa wa Dodoma, wakisikiliza mawaidha wakati wa swala ya Eid El Fitri, katika msikiti wa Nughe, jijini humo, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Umati wa waumini wa dini ya Kiislamu, wakiwa katika swala ya Idd El Fitri katika msikiti mkuu wa Ijumaa, Muheza mjini, mkoani Tanga jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Waumini wa dini ya Kiislamu, wakichagua vazi la kanzu, baada ya kumaliza swala ya Eid El Fitri, katika msikiti mkuu wa Ijumaa, mjini Muheza, mkoani Tanga jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (katikati), akishiriki swala ya Eid El Fitri, katika msikiti wa Ijumaa wa Kiombamvua, Zanzibar jana. **PICHA: OMPR – ZNZ**

HABARI KIMATAIFA

## Waliofariki kwa corona Marekani wafikia 100,000

**WASHINGTON, Marekani**

RAIA wa Marekani wameanza kuminika katika fukwe za bahari kutokana na hali nzuri ya hewa.

Rais wa nchi hiyo, Donald Trump naye alijumuika uwanjani kucheza gofu, lakini nchini humo vifo vya watu waliofariki kwa corona vikifikia 100,000.

Marekani imeorodhesha vifo 1,127 zaidi kutokana na ugonjwa wa virusi vya corona na hadi kufikia sasa jumla ya vifo imefikia 100,000, huku kiwango cha maambukizo kikifikia 1,621,658.

Rais Trump alionekana akicheza gofu huku wakazi wa Marekani wakijianika juani wakati hatua za vizuizi zikianza kulegezwa nchini humo.

Rais Trump ambaye anataka makanisa, masinagogi na misikiti kuruhusiwa haraka kuendesha ibada, hakuwa amevaa barakoa wakati alipokuwa akicheza gofu, na hata wachezaji wenzake nao hawakuvaa barakoa.

Wakati huo huo, Wamarekani wengi walio na shauku na sikukuu ya mashujaa wikiendi hii wamemiminika kwenye fukwe na maeneo ya nje.

Siku hiyo huadhimishwa Jumatatu ya mwisho ya mwezi Mei kila mwaka kuwakumbuka wale waliopoteza maisha wakihudumu katika majeshi ya Marekani.

Nako nchini Hispania inatarajia kufungua tena milango kwa ajili ya watalii wa nje kuanzia mwezi Julai, baada ya serikali kuahidi kwamba itahakikisha usalama wa wageni na wenyeji.

Zaidi ya watalii milioni 80 huwa wanaitembelea Hispania kwa mwaka. Mnamo mwaka uliopita, Wajerumani milioni 11 walifanya utalii katika nchi hiyo ambayo sasa inahofia kwamba takwimu hizo zikaporomoka.

**DW**

**Nako nchini Hispania inatarajia kufungua tena milango kwa ajili ya watalii wa nje kuanzia mwezi Julai, baada ya serikali kuahidi kwamba itahakikisha usalama wa wageni na wenyeji.**

# Waislamu duniani washerehekea Eid El Fitr kwa tahadhari corona

**RIYADH, Saud Arabia**

WAISLAMU jana walisherehekea sikukuu ya Eid el-Fitr, huku wengi wakiwa chini ya vizuizi vilivyowekwa na mataifa kukabiliana na kuenea kwa virusi vya ugonjwa wa corona.

Sikukuu ya Eid ni moja ya sherehe muhimu kwenye kalenda ya uislamu, huashiria kumalizika kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na huadhimishwa kwa ibada ya swala, dhifa za chakula na manunuzi ya zawadi pamoja na mavazi.

Hata hivyo, mwaka huu sherehe za Eid zimeandamwa na janga la corona, huku nchi nyingi duniani zikitangaza kurejesha vizuizi ambavyo kwa sehemu vililegezwa wakati wa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Katika hali ya kupunguza msisimuko wa sherehe hizo, mataifa kadhaa ikiwamo Saudi Arabia, Uturuki, Misri na Syria yamepiga marufuku ibada za umati, moja ya tukio muhimu katika sikukuu ya Eid, kwa lengo la kuzuia kusambaa virusi vya corona.

SAUDI ARABIA

Maeneo mawili tukufu kwa dini ya Uislamu, serikali ilitangaza kuwa swala ya Eid itafanyika kwenye misikiti mikuu ya Makka na Madina bila kuhudhuriwa na waumini.

Msikiti mkuu mjini Makka hautembelewi na waumini tangu mwezi Machi na ukimya umegubika eneo la Kaaba - tufe kubwa jeusi ambalo waumini wote wa kiislamu hufanya ibada kwa kuzingatia mwelekeo wa mahali lilipo.

Saudi Arabia imeanza marufuku kali ya kutotembea nje itakayodumu kwa muda wa siku tano baada ya maambukizo ya corona kuongezeka zaidi ya mara tatu na kufikia visa 68,000 tangu kuanza kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Msikiti wa Al-Aqsa uliopo mjini Jerusalem, ambao ni wa tatu kwa utukufu ndani ya uislamu utafunguliwa tena kwa waumini kuutumia baada ya sikukuu ya Eid.

LEBANON

Taifa lenye idadi kubwa ya waislamu wa madhehebu ya Sunni serikali ilitangaza kufunguliwa kwa misikiti kwa ibada ya swala ya Ijumaa pekee.

Lakini waumini walilazimika kupimwa joto la mwili na kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya virusi vya corona.

Wakati huo huo waislamu barani Asia kuanzia Indonesia, Pakistan, Malaysia hadi Afghanistan walifurika kwenye masoko kwa maandalizi ya sikukuu ya Eid na kusababisha ukiukwaji mkubwa wa masharti yaliyowekwa kupambana na virusi vya corona.

INDONESIA

Taifa lenye idadi kubwa ya waislamu duniani, watu wanajaribu kuwatumia walanguzi na nyaraka bandia za kusafiria ili kukwepa marufuku zilizowekwa mwishoni mwa mwezi wa Ramadhan, mwenendo unaotishia kuongeza maambukizo.

**DW**



Waumini wa dini ya Kiislamu nchini Saud Arabia wakiwa katika ibada ya Sikukuu ya Eid El-Fitr iliyoadhimishwa duniani kote jana. **PICHA: DW**

# Kanisa lafungua milango kwa Waislamu kuswali

**BERLIN, Ujerumani**

UWAPO wa ugonjwa wa virusi vya corona kumesababisha kanisa moja mjini Berlin Ujerumani, kufungua milango na kuwaruhusu waumini wa dini ya Kiislamu kufanya ibada yao.

Hatua hiyo imetokana na waumini wa dini hiyo kutotosha katika msikiti, baada ya kutolewa utaratibu mpya wa kutokaribiana.

Ujerumani iliruhusu sehemu za kuabudiwa kufunguliwa Mei 4, mwaka huu, lakini kwa masharti kuwa watu wakae kwa umbali wa mita 1.5.

Hatua hiyo ilisababisha msikiti wa Dar Assalam uliopo mjini Neukölln kushindwa kumudu vigezo hivyo kwa sababu hauwezi kutosha kutokana na uwapo wa idadi kubwa ya waumini.

Lakini Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Martha katika mji wa Kreuzberg, Ujeruamani lilitoa ruhusa kwa Waislamu kufanya ibada zao Ijumaa na katika wiki ya mwisho ya mfungo wa Ramadhani.

Kwa kipindi cha mwezi mzima wa Ramadhan, Waislamu walikuwa katika mfungo wa Mwezi Mtukufu, na kuanzia jana wameanza kusherehekea sikukuu ya Iddi.

Kwa kawaida familia na marafiki huwa wanajumuika kwa pamoja kuhitimisha mfungo kwa kusherehekea na kujumuika katika sala za pamoja, lakini kwa mjini Berlin na hata maeneo mengi duniani sherehe hizo bado zimeathirika.

"Ni ishara njema na inaleta furaha kwa wakati huu na inaleta furaha katikati ya janga, mlipuko huu umetufanya kuwa jumuiya moja. Majanga yamewafanya watu wawe kitu kimoja."

"Ni hisia ya ajabu kwa sababu ya ala za muziki na picha za ukutani ni kitu tofauti, Lakini unapoangalia, unaposahau kidogo. Hii ni nyumba ya Mungu. Hakuna kitu ambacho kinawakilisha swala za kiislamu," alisema Samer Hamdoun, mmoja wa waumini katika msikiti huo na kuongeza:

"Hata wachungaji wa kanisa wamehudhuria swala hizo. Nilitoa hotuba Ujerumani, wakati wa maombi, nilikuwa naweza kusema ndio, ndio, ndio kwa sababu tunamatatzio ya kufanana na tunataka kujifunza kutoka kwenu. Na hisia hiyo ni nzuri kati yetu." **BBC**



# WENGER AFURAHI LIVERPOOL KUSHINDWA KUFIKIA REKODI

**LONDON, England**

ARSENE Wenger amekubali kwamba, alifurahia kuona Liverpool wakishindwa kuweka rekodi ya kutofungwa hadi kumalizika kwa Ligi Kuu ya England msimu huu wa 2019/2020.

Liverpool walikuwa hawajafungwa katika mechi 27 za ligi na walikuwa wanayemelea kufikia rekodi ya Arsenal ya msimu wa 2003-04, wakati waliposhinda taji hilo bila kupoteza mchezo wowote.

Hata hivyo, vijana wa Jurgen Klopp walichapwa 3-0 na Watford Februari, wakishindwa kufikia rekodi ya kikosi cha Wenger.

Mfaransa huyo alisema alifurahia kuona Arsenal imebaki kuwa ndiyo timu pekee ambayo ilitwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya England bila kupoteza mchezo.

"Ndio, kilikuwa kiwango cha juu. Mara zote tulipenda kuhakikisha tunafanikiwa jambo fulani," alisema Wenger akiiambia beIN SPORTS.

"Wao (Liverpool) wangeweza kufuata nyayo, lakini inaonyesha kuwa ni ngumu sana kufikia rekodi hiyo. Siku ile nilipata ujumbe mwingi kutoka kwa mashabiki wa Arsenal."

Liverpool walikuwa wanaongoza kileleni mwa msimamo kwa tofauti ya pointi 25 wakati ligi hiyo ilipositmama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

# POCHETTINO SASA NJIA NYEUPE NEWCASTLE

**NEWCASTLE, England**

MAURICIO Pochettino ana "ofa nzuri" mezani kutoka kwa Newcastle United na uhamisho huo "una uwezekano thabiti", kwa mujibu wa Ossie Ardiles.

Pochettino amekuwa nje ya uongozi wa soka tangu alipofukuzwa kule Tottenham Novemba mwaka jana, ikiwa ni miezi mitano tu tangu aiongoze kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo wa zamani wa Argentina mara kwa mara amekuwa akihusishwa na Real Madrid na Manchester United katika misimu ya hivi karibuni, lakini Zinedine Zidane na Ole Gunnar Solskjaer wanaonekana bado wapo sana kwenye nafasi zao.

Kuwaniwa kwenda kuinoa Newcastle ndio kumepamba vichwa vya habari wiki za hivi karibuni, huku klabu hiyo ikiripotiwa inakaribia kununuliwa kwa pauni milioni 300 na kampuni ya nchini Saudi Arabia, Public Investment Fund.

Kocha wa sasa wa Newcastle, Steve Bruce amesisitiza angependa kuchukua nafasi ya kuwamo kwenye zama mpya, bado Pochettino amezungumzia uwezekano wa kubaki England na kuinoa klabu nje ya 'sita bora' kwenye Ligi Kuu ya England.

Hata hivyo, Ardiles mchezaji wa zamani wa Tottenham na kocha wa zamani wa Newcastle - amebainisha rafiki yake huyo sasa anafikiria ofa baada ya kumalizana kabisa na Spurs.

"Mauricio anajisikia vizuri kuwa England," alisema Ardiles akiliambia gazeti la Mirror. "Anahusishwa na Newcastle United.

"Na wakati alipozungumza nao moja kwa moja na klabu ile, walimpa ofa nzuri.

"Mauricio alikuwa na (mkataba wa kimahusiano) na Tottenham, lakini Jumanne walimalizana na yupo huru.

"Kwa njia hii, atasikiliza tena ofa, lakini uhamisho wa kwenda Newcastle unauwezekano thabiti kwa yeye kufanya tena kazi."

# Gotze kuondoka Dortmund

**DORTMUND, Ujerumani**

MARIO Gotze ataondoka Borussia Dortmund mwishoni mwa msimu huu, mkurugenzi wa michezo, Michael Zorc amethibitisha.

Kiungo huyo alithibitisha Aprili kwamba alikuwa na mpango wa kuondoka hapo kwenye dimba la Signal Iduna Park wakati akifikiria kwenda sehemu nyingine, ingawa Ofisa Mtendaji Mkuu, Hans-Joachim Watzke baadaye alibainisha kwamba, Gotze anaweza kusaini mkataba mpya.

Kocha Mkuu, Lucien Favre aliyaweka majaliwa ya Gotze shakani wakati alipokubali kuwa mchezaji huyo hatafiti kwa mfumo wake.

Akizungumza kabla ya mchezo wa Jumamosi wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, dhidi ya Wolfsburg, Zorc alithibitisha Gotze ataondoka akiwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu wa 2019-20.

"Tutamaliza kufanya kazi na Mario kipindi cha majira ya joto kinachokuja," alisema Zorc akiiambia Sky.

"Yamefanyika maamuzi ya kukubalika baada ya majadiliano. Mario ni mzuri."

Gotze alirudi Dortmund mwaka 2016 baada ya kuondoka katika klabu yake hiyo ya utotoni na kujiunga Bayern Munich alikokaa kwa miaka mitatu.

## HABARI MICHEZO




# PSG KUMSAJILI MOJA KWA MOJA ICARDI

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain imetoa ofa kwa Inter Milan ya euro milioni 50, ili kumnunua moja kwa moja, Mauro Icardi, kwa mujibu wa Sky Sports.

Icardi anacheza kwa mkopo kule PSG akitokea Inter na amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi tangu atue hapo jijini Paris mwanzoni mwa msimu huu.

Majaliwa ya Icardi pale Inter yanaonekana kutokuwapo hasa ikizingatiwa kuwa kocha, Antonio Conte alishabainisha kwamba mchezaji huyo hana nafasi katika mipango yake.

Lakini sasa Icardi anatakiwa kubakia Paris, ambako raia huyo wa Argentina ametumia kipindi chote cha msimu huu wa 2019-20 akicheza huko kwa mkopo.

"PSG kwa sasa wanaona Icardi atafiti kwenye mipango yao ya baadaye na kwamba wanataka kumsajili kwa mkataba wa kudumu," liliandika gazeti la France Football.

Thamani ya Icardi ni euro milioni 70, lakini PSG wanajaribu kuishawishi Inter wamsajili kwa euro milioni 50, huku pia Juventus wakiripotiwa kumuwania.

# Higuain kustaafia soka River Plate

**TURIN, Italia**

GONZALO Higuain hana uhakika kama ataondoka Juventus kwenda kucheza River Plate, ingawa mshambuliaji huyo angependa kustaafu soka katika klabu yake hiyo ya utotoni.

Higuain amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kuondoka kwa mabingwa hao wa Serie A, Juve - ili arudi kwa miamba wa Argentina, River.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, pia ametajwa kuwaniwa na klabu za Ligi Kuu ya Marekani (MLS), LA Galaxy na DC United akiwa ametokea kwenye akademi ya vijana ya River mwaka 2005 kabla ya kuhamia kwa miamba wa LaLiga, Real Madrid miaka miwili baadaye.

Higuain ameelezea kuhusu majaliwa yake na kuzungumzia kuungana na River, akiiambia TyC Sports: "River ni klabu ambayo ilinipa mimi kila kitu, kwa kuniendeleza na kuniachia ninunuliwe na Real Madrid, lakini kwa sasa sijui nini kinaendelea. Kichwa changu kipo hapa Turin.

"Timu ya (Marcelo) Gallardo inavutia, wana ubora, nguvu na kila kitu. Ukweli ni kwamba ni timu iliyokamilika, na ningependa kumalizia soka langu pale."

Kabla ya msimu kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, Higuain alifunga mabao matano katika mechi 23 alizocheza.

Kwa ujumla, Higuain amefunga mabao nane katika mashindano yote msimu huu kwa kikosi hicho cha Maurizio Sarri.



# Setien ataka kumnoa Neymar pale Barca

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Quique Setien amesema "angependa" kumnoa nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar pale Camp Nou.

Neymar aliondoka Barca kwenda PSG kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222 katika uhamisho wa mwaka 2017, lakini mshambuliaji huyo wa Brazil ameendelea kuhusishwa na mpango wa kurudi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alishindwa kurudi kule Barca mwanzoni mwa msimu wa 2019-20 na ameripotiwa kuwaniwa tena.

"Bila shaka yoyote, ningependa kuwa kocha wa Neymar siku moja," alisema kocha mkuu wa Barca, Setien akiiambia beIN SPORTS.

"Kwa uhakika kabisa. Yeye ni mchezaji ambaye yupo daraja la juu kabisa, hakuna mwenye shaka na hilo.

"Nimeshatimiza ndoto ya kumnoa mchezaji bora zaidi duniani, ambaye ni Leo (Messi). Na kwa yeyote atakayeweza kuja hapa, tutaona, lakini nitafurahi sana."

Tangu kuondoka Barca kwenda PSG, Neymar ameshinda mataji matatu mfululizo ya Ligue 1, pamoja na Coupe de France, Coupe de la Ligue na Trophee.

Neymar amefunga mabao 13 ya ligi kabla ya msimu kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona na PSG walipewa ubingwa baada ya ligi hiyo kufutwa rasmi msimu huu.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Barca si mchezaji pekee anayehusishwa na miamba hao wa Hispania.

Straika wa Inter Milan, Lautaro Martinez amekuwa pia akitajwa kuwaniwa na Barca, huku kiungo wa Juventus, Miralem Pjanic akiripotiwa kutakiwa pale Camp Nou.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# COUTINHO NDIYO BASI TENA BAYERN

Kipengele cha mkataba kimemalizika muda wake na hatujakiongeza, tunakwenda...

**MUNICH, Ujerumani**

MWENYEKITI wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge amebainisha kwamba mabingwa hao wa Bundesliga hawana mpango wa kumsajili moja kwa moja Philippe Coutinho na kipengele kilichopo kwenye mkataba wake kwa sasa kimemalizika muda wake.

Coutinho alijiunga na Bayern kwa mkopo wa muda mrefu kutoka kwa mabingwa wa LaLiga, Barcelona mwanzoni mwa msimu 2019-20, lakini amekuwa na wakati mgumu wa kujiimarisha kiwango chake pale Munich.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alitua hapo huku kukiwa na kipengele cha kumnunua kwa euro milioni 120, lakini Bayern hawana mpango huo, ingawa Rummenigge hajafunga mlango kwa Coutinho.

"Kipengele cha mkataba kimemalizika muda wake na hatujakiongeza," alisema Rummenigge akiliambia jarida la Ujerumani la Der Spiegel.

"Tunakwenda kupanga kikosi chetu kwa ajili ya msimu ujao na tutaangalia kama atakuwa na nafasi ya kucheza na sisi au la."

Coutinho ameshindwa kuwa kwenye kiwango chake kama ilivyokuwa wakati akicheza kule Liverpool na kununuliwa na Barca mwaka 2018.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amefunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho sita katika mechi 22 za Bundesliga alizoichezea Bayern msimu huu.

## KWA UFUPI

### POGBA, JUVE WATETA
WAKALA wa Paul Pogba, Mino Raiola ameanza mazungumzo na Juventus kuhusu uhamisho wa majira ya kipindi cha joto, lakini Real Madrid na Paris St-Germain zote zinamuwania kiungo huyo wa Manchester United mwenye umri wa miaka 27. ***(Le10sport)***

### BAYERN KUITIBULIA UNITED
KLABU ya Bayern Munich inaweza kuingia kwenye mipango ya kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer kumsajili winga wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20. ***(Sun)***

### BARCA KUUZA SITA
BARCELONA imeripotiwa inampango wa kuwauza wachezaji sita kipindi cha majira ya joto ili kutatua tatizo la kifedha lililoikumba klabu hiyo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. ***(Marca)***

### ARSENAL KWA TAGLIAFICO
KLABU ya Arsenal inafukuzia kumsajili mlinzi wa Ajax, Nicolas Tagliafico mwenye umri wa miaka 27, kwa pauni milioni 20, baada ya nyota huyo wa Argentina kuonyesha kiwango cha juu kwa miamba hao wa Uholanzi wakati walipotinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita. ***(Mirror)***

### AGUERO YUPO SANA CITY
WAKALA wa Sergio Aguero amekanusha madai kwamba mshambuliaji huyo wa Manchester City mwenye umri wa miaka 31, anaweza kuondoka Etihad kipindi hiki cha majira ya joto, huku uvumi ukimhusisha na kurudi Argentina. ***(Mirror)***

### WILLIAN NJIAPANDA CHELSEA
KIUNGO wa Chelsea, Willian mwenye umri wa miaka 31, amesema kukataa kwa klabu hiyo kumwongezea mkataba wa miaka mitatu kumemwacha akiwa kwenye hali "ngumu". ***(Esporte Interativo, via Metro)***

### KOULIBALY AKARIBIA UTD
KLABU ya Manchester United kwa sasa ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumsajili mlinzi wa kati wa Napoli, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 28, baada ya PSG, Barcelona na Real Madrid kujitoa kwenye mbio za kumwania. ***(Sun)***

### MAITLAND KUSEPA ARSENAL
KIUNGO, Ainsley Maitland-Niles mwenye umri wa miaka 22, anatarajia kuondoka Arsenal wakati dirisha la kipindi cha majira ya joto litakapofunguliwa baada ya kushindwa kumshawishi kocha wake mpya, Mikel Arteta. ***(Star)***

### HAALAND BADO MIWILI
REAL Madrid na Manchester United huenda wakatakiwa kusubiri mpaka miaka miwili ijayo ili kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 19, kwa kuwa mkataba unaomruhusu kuuvunja kwa dola milioni 75, unasema anaweza kuuzwa kuanzia mwaka 2022 na si chini ya hapo. ***(Evening Standard)***

### RABIOT ATETA UNITED
MANCHESTER United imefanya mazungumzo na wakala wa kiungo wa Juventus, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 25, huku pia Arsenal na Everton zikimwania. ***(Mirror)***

### MADRID KUMSAJILI AJER
KLABU ya Real Madrid inafikiria kumsajili mlinzi wa Celtic na timu ya Taifa ya Norway, Kristoffer Ajer mwenye umri wa miaka 22, baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye Ligi Kuu ya Scotland. ***(Mundo Deportivo)***

# WASAUZI, YANGA MBIO MOJA KWA BIGIRIMANA

**Na Saada Akida**

MIPANGO ya Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, kuipata huduma ya mshambuliaji wa Namungo FC, Bigirimana Blaise huenda ikawa migumu kutokana na klabu moja ya Afrika Kusini kuingia katika mbio za kuisaka saini ya Mrundi huyo, imefahamika.

Meneja wa mchezaji huyo, Mohammed Kisoki, ameliambia Nipashe jana jijini Dar es Salaam kuwa, amepata ofa nyingi ndani na nje nchini ikiwamo Afrika Kusini.

Alisema kwa hapa nchini hakuna timu iliyomfuata moja kwa moja kwa ajili ya kufanya mazungumzo zaidi ya klabu yake ya Namungo ambayo anahitaji kumwongezea mkataba.

"Kuna ofa kutoka sehemu mbalimbali ikiwamo Afrika Kusini, kuna timu imeonyesha nia, tunachoangalia zaidi ni maslahi pamoja na mikataba yao," alisema Kisoki.

Alisema mteja wake anaangalia maslahi na endapo wakiafikiana vizuri na Namungo, anaweza kusalia ndani ya kikosi cha timu hiyo au kwenda Afrika Kusini.

"Suala la Yanga siwezi kuliongelea maana hawajaja rasmi kwangu, hivyo nina imani viongozi wanajua kanuni juu ya mchezaji mwenye mkataba kufuata njia zote," alisema.

Meneja huyo alisema mkataba wa mteja wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, hivyo milango ipo wazi kwa timu ambayo inayohitaji huduma ya mteja wake huyo.

Kuna tetesi kwamba Yanga wamekuwa wakihitaji huduma za Blaise kwa ajili ya msimu ujao, ingawa mazungumzo rasmi bado hayajafanyika.

# Eymael kurejea Yanga wiki hii

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umepanga kutuma tiketi kwa makocha wao, Mbelgiji Luc Eymael na msaidizi wake raia wa Afrika Kusini, Riedoh Berdien waliopo nje ya nchi ili kurejea kabla ya Juni Mosi, mwaka huu.

**Wiki iliyopita serikali ilitangaza ruksa ya kurejea kwa Ligi Kuu, Kombe la FA, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli kueleza kuridhishwa na kushuka kwa kasi ya maambukizo ya virusi vya corona nchini.**

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, ameliambia Nipashe jana kuwa, wamepanga kuwatumia tiketi za ndege makocha hao mapema iwezekanavyo ili kuwahi kurejea nchini.

Alisema kwa sasa wanashughulikia taratibu hizo ili makocha wao waweze kurejea mapema na kuanza maandalizi ya ligi hiyo, ila kwa sasa kikosi chao kitakuwa chini Boniface Mkwasa.

"Tumepokea kwa furaha taarifa za kurejea kwa michezo, tunaamini ligi itaendelea ili kumalizia michezo tuliyoibakisha kabla ya kuuanza msimu mpya, tumepanga kuwakatia tiketi makocha wetu haraka baada ya Rais Magufuli kutangaza kuwa ndege kutoka mataifa mengine zitaanza kuruhusiwa kuingia nchini," alisema Mwakalebela.

# Kilichomuua Babu Njenje hiki hapa

**Na Adam Fungamwango**

MWANAMUZIKI Mkongwe wa bendi ya Kilimanjaro, Mabrouk Hamisi Omari, maarufu kama 'Babu Njenje' amefariki dunia jana alfajiri jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa mwanamuziki mwenzake wa bendi hiyo, John Kitime, Babu Njenje alifariki dunia nyumbani kwake Mtaa wa Mindu, Upanga jijini Dar es Salaam, baada ya kusumbuliwa kwa muda mrefu na ugonjwa wa kiharusi.

"Kwa muda sasa alikuwa amesimama kupanda jukwaani kutokana na matatizo yake ya kiafya, leo (jana) alfajiri ametutoka na msiba uko nyumbani kwake Upanga," alisema Kitime.

Mazishi ya mwanamuziki huyo aliyejizolea umaarufu mkubwa mwishoni mwa miaka ya '90 na mwanzoni mwa miaka ya 2000 kwa nyimbo zake zenye mahadhi ya mduara, yalitarajiwa kufanyika jana saa 10:00 jioni kwenye makaburi ya Kisutu jijini Dar es Salaam.

**Babu Njenje alikuwa ndiye mwimbaji kiongozi wa bendi hiyo na alitamba kwa kuimbisha nyimbo kama 'Njenje' ambao ulitamba sana miaka ya '90 na ndiyo uliosababisha bendi ya Kilimanjaro kuitwa 'Wana Njenje', huku marehemu naye akipachikwa jina la Babu Njenje kutokana na kuuimba wimbo huo wenye mahadhi ya mduara kwa ustadi mkubwa.**

Mbali na wimbo huo, Babu Njenje pia alitunga na kuimba nyimbo zingine nyingi zilizompatia sifa yeye binafsi na bendi yake kama 'Kinyaunyau', 'Ndembele', 'Kachiri', na nyingine nyingi.

Marehemu ameacha mke na watoto wawili.

KIKAZI ZAIDI...




Kiungo wa timu ya Wanaume ya Yanga, Mnyarwanda Haruna Niyonzima, wakipozi pamoja na beki wa timu ya Wanawake ya Simba, Fatuma Issa 'Densa', baada ya mazoezi ufukweni mwa Bahari ya Hindi, jijini Dar es Salaam juzi, katika kipindi hiki klabu zao zikiwa zimesitisha mazoezi ya vikosi kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19). **MPIGAPICHA WETU**

# Mwambusi atoa neno ligi ikirejea

**Na Shufaa Lyimo**

ALIYEWAHI kuwa Kocha Mkuu wa Mbeya City, Juma Mwambusi, amesema amefurahi kuona Ligi Kuu ikirejea baada ya wachezaji kupumzika kwa muda mrefu kutokana na likizo iliyosababishwa na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19), lakini akaonya tahadhari haina budi kuendelea kuchukuliwa.

Ligi Kuu pamoja na michezo yote nchini ilisimama tangu Machi 17, mwaka huu kufuatia agizo la serikali baada ya mlipuko wa virusi vya corona nchini na duniani kote, lakini wiki iliyopita Mei 21, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, aliruhusu ligi hiyo kurejea kuanzia Juni Mosi baada ya kuridhishwa na kushuka kwa kasi ya maambukizo ya virusi vya corona nchini.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwambusi alisema kufuatia kutangazwa kurejea kwa ligi hiyo, kumefurahisha wadau mbalimbali wa soka hapa nchini akiwamo yeye binafsi.

"Ni jambo jema kuanza kwa ligi hofu za Watanzania zitapungua, vilevile bingwa atapatikana kihalali," alisema Mwambusi.

Mwambusi aliongeza kuwa wachezaji wanapaswa kucheza kwa tahadhari pindi watakaporejea uwanjani, kwa madai kwamba ugonjwa wa Covid-19 bado upo.

Michezo
Jumatatu Mei 25, 2020
Nipashe



Coutinho ndiyo basi tena Bayern

HABARI UK 22

IKO HIVI...



Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingisa. **PICHA: SIMBA**

## Morrison aitaka Ligi Kuu hata leo

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya serikali kuruhusu Ligi Kuu Bara kurejea, winga mshambuliaji wa Yanga, Mghana Bernard Morrison, amesema anatamani ligi hiyo ianze hata leo ili aendelee kuonyesha vitu vyake uwanjani.

Akizungumza na Nipashe jana Morrison, alisema ameutumia vizuri muda wote wa mapumziko kujinoa ili kujiweka sawa ikiwa ni pamoja na kufuata maelekezo muhimu kutoka kwa walimu wake.

Alisema amefurahishwa na kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Dk. John Magufuli, kuamua michezo irudi pamoja na majukumu mengine.

"Nimefurahi kurudi uwanjani, 'nimemisi' mashabiki wangu kwa kipindi kirefu, naahidi kurudi kwa kasi ili kuipa ushindi timu yangu," alisema Morrison ambaye ameteka hisia kubwa za mashabiki wa Yanga kwa sasa.

Alisema lengo lake ni kutoa burudani kwa mashabiki pamoja na uongozi wake kuhakikisha anaongeza kasi uwanjani ya kupachika mabao.

"Mpira ni kazi yangu, lazima nijitume kama kawaida kwa lengo la kutimiza malengo yangu ambayo nimejiwekea kwa muda mrefu," alisema.

Alisema amefuata kwa umakini maelekezo aliyokuwa anapewa na walimu wake na kudai anashukuru anaendelea vizuri kiafya.

"Tuzidi kufuata maelekezo ya kujikinga na virusi vya corona kama wataalamu wanavyosisitiza, hata tutakapokuwa uwanjani tuwe na tahadhari," alisisitiza.

# SIMBA SC YAANIKA MKAKATI WA USAJILI

Yaeleza pia malengo yao Ligi Kuu, FA Cup, Kagere, Chama na Kahata kurejea leo...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kuhusishwa na nyota kibao kuelekea dirisha la usajili msimu ujao, uongozi wa Klabu ya Simba umeomba subira kwa mashabiki wao, huku ukieleza unataka kufanya mambo mazuri na utaanika kila kitu kadri utakavyokuwa ukisajili.

Simba na Yanga zimeelezwa kuanza mipango ya kusuka vikosi vyao kimyakimya, huku zikihusishwa na wachezaji kibao akiwamo beki wa kati wa Coastal Union ya Tanga, Bakari Mwamnyeto, lakini mabingwa watetezi hao wa Ligi Kuu Bara wamewataka mashabiki wao kutuliza mzuka kwa kuwaeleza bado hawajaanza mbio hizo rasmi.

Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingisa, akizungumza jijini Dar es Salaam, amesema kwa sasa wanaendelea kwanza kufanyia kazi wachezaji waliopo kwa kuwaongeza mikataba mipya na mchezaji yeyote ambaye watamsajili watatoa taarifa.

"Mashabiki wetu watupe muda na nafasi kufanya kazi nzuri kwenye usajili. Tunaendelea kufanyia kazi kwa wachezaji waliopo kuongeza mikataba mipya na mchezaji yeyote ambaye tutamsajili tutatoa taarifa. Kwa sasa hatujasajili mchezaji yeyote," alisema Mazingisa.

Kuhusu kurejea kwa wachezaji waliopo nje ya nchi baada ya serikali kuruhusu Ligi Kuu kurejea rasmi kuanzia Juni Mosi, mwaka huu, Mazingisa alisema nyota hao wataanza kutua nchini kuanzia leo Jumatatu.

"Wachezaji wetu wote ambao wapo nje ya Tanzania, tunawasiliana nao na mmoja kati ya hao atakuwapo nchini Jumatatu [leo]. Wengine tunatarajia watakuwapo nchini kabla hatujaanza mazoezi," alisema huku akieleza kuwa mazoezi hayo yataanza rasmi keshokutwa, Jumatano.

Wachezaji wa Simba walioko makwao nje ya nchi ni mshambuliaji Mnyarwanda Meddie Kagere, kiungo Mzambia Clatous Chama na winga Mkenya Francis Kahata.

Aidha, Mazingisa alisema mikakati yao kwa sasa ni kushinda kwanza ubingwa wa Ligi Kuu pamoja na Kombe la FA, ili kuwa na uhakika wa kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao.

"Lazima tujikite kuhakikisha tunashinda Ligi Kuu na FA. Hiyo ndio dhamira yetu kwa sasa," alisema.

Hadi Ligi Kuu inasimama Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19, Simba ipo kileleni ikiwa na pointi 71, ikifuatiwa na Azam FC yenye ama 54 baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 28, Yanga iliyopo mchezo mmoja nyuma ina pointi 51 katika nafasi ya tatu.

Tayari wizara yenye dhamana na michezo nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) pamoja na Bodi ya Ligi (TPLB), wamekubaliana ligi zilizoruhusiwa kurejea ambazo ni Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili, zichezwe katika kituo kimoja badala ya utaratibu wa nyumbani na ugenini.

Kwa mujibu wa maamuzi yaliyofikiwa Ligi Kuu itachezwa jijini Dar es Salaam katika Uwanja wa Taifa, Uhuru na Azam Complex, wakati mechi za Ligi Daraja la Kwanza na la Pili zitachezwa jijini Mwanza kwenye Uwanja wa CCM Kirumba na Nyamagana.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >